Environment, Natural Resources and Food



MAFUNZO YA UANDAAJI MIPANGO SHIRIKISHI YA MATUMIZI BORA YA ARDHI NA RASLIMALI NYINGINEZO KWA VIONGOZI WA VIJIJI, KATA NA WILAYA

(Wilaya ya Namtumbo na Tunduru, Mkoa wa Ruvuma)

UKUMBI WA DON-BOSCO, KANISA KATOLIKI SONGEA, 5 – 10 NOVEMBA 2007

Internationale Weiterbildung und Entwicklung gGmbH

Capacity Building International, Germany

Selous-Niassa Wildlife Corridor

MAFUNZO YA UTAYARISHAJI MIPANGO SHIRIKISHI YA MATUMIZI BORA YA ARDHI NA RASILIMALI NYINGINEZO

KWA

VIONGOZI WA VIJIJI NA WILAYA NA WANANCHI WA

WILAYA ZA NAMTUMBO NA TUNDURU

MKOA WA RUVUMA

UKUMBI WA KANISA KATOLIKI MANISPAA YA SONGEA

5 – 10 NOVEMBA 2007

IMETAYARISHWA NA:

Dr. Fred Lerise	**Chuo kikuu cha Ardhi**
Dr. Jafar Kideghesho	**Chuo kikuu cha Kilimo cha Sokoine**
Mr. Ally Namangaya	**Chuo kikuu cha Ardhi**
Mr. Daniel Msangi	**Chuo kikuu cha Ardhi**
Mr. Benedict Malele	**Chuo kikuu cha Ardhi**
Mr. Abdi Ka'Bange	**Chuo kikuu cha Ardhi**

YALIYOMO

SIKU YA KWANZA 1
1.1 Utangulizi wa mafunzo na ufunguzi 1
1.2 Matarajio ya washiriki 6
1.3 Malengo na mbinu za mafunzo 8
1.4 Sera mbali mbali na dhana ya ushirikishwaji 8

SIKU YA PILI 13
2.1 Uhusiano/uwiano mlalo wa mipango mbalimbali (horizontal integration) 13
2.2 Uhusiano/uwiano ngazi wa mipango mbalimbali (vertical integration) 16
2.3 Muundo wa kisheria na kitaasisi 18
2.4 Hatua za kuandaa Mpango shirikishi 19
2.5 Hatua za kupitisha na kutekeleza Mpango shirikishi 22
2.6 Wajibu wa watendaji katika mipango shirikishi na usimamizi wake 23
2.7 Majumuisho 24

SIKU YA TATU 26
3.1 Uhakiki wa rasilimali (Resource Assessment) 26
3.2 Kutenga maeneo kwa matumizi mbali mbali (Resource use options) 27
3.3 Majumuisho 32

SIKU YA NNE 33
4.1 Kuwasilisha mpango kwenye mkutano mkuu 33
4.2 Utekelezaji wa mpango 34
4.3 Kuibua miradi kutoka mpango wa matumizi bora ya ardhi 34
4.4 Majumuisho 38

SIKU YA TANO 40
5.1 Mchakato wa kuanzisha mradi wa hifadhi ya jamii (WMA) 40
5.2 Changamoto katika kuandaa, kupitisha na kutekeleza sheria ndogo 41
5.3 Kutunga sheria ndogo (Resource persons) 43
5.4 Mpango wa utekelezaji (Action plan) 45
5.5 Majumuisho 46

SIKU YA SITA 48
6.1 Mpango wa mfano (Ripoti) 48
6.2 Mpango wa mfano (Ramani) 50
6.3 Tathmini ya mafunzo 51
6.4 Kufunga mafunzo 51

VIAMBATANISHO 53
Kiambatanisho Namba 1: Ratiba ya mafunzo 53
Kiambatanisho Namba 2: Orodha ya washiriki wilaya ya Namtumbo 57
Kiambatanisho Namba 3: Orodha ya washiriki wilaya ya Tunduru 58
Kiambatanisho Namba 4: Tathmini ya mafunzo kwa maswali mbali mbali 59
Kiambatanisho Namba 5: Orodha ya Nyaraka Rejea 63

SIKU YA KWANZA **JUMATATU 5/11/2007**

1.1 Utangulizi wa mafunzo na ufunguzi

Kujiandikisha

Siku ya kwanza ya mafunzo ilianza kwa washiriki kujiandikisha ili kuratibu mahudhurio. Washiriki walijiandikisha kwa kufuata wilaya waliyotoka. Wilaya ya Namtumbo ilikuwa na washiriki 50 na wilaya ya Tunduru ilikuwa na washiriki 31 waliotoka katika Vijiji, Kata, Tarafa na wataalam wa Wilaya. Kwa ujumla washiriki wa mafunzo walikuwa 81. Idadi ya washiriki na sehemu walizotoka ni kama invyooneshwa katika jedwali Namba 1.1. Orodha kamili ya washiriki inaoneshwa katika kiambatanisho Namba 2 na namba 3.

Jedwali Na 1.1: Washiriki wa mafunzo na Taasisi walizotoka

Wilaya ya Namtumbo		**Wilaya ya Tunduru**	
Taasisi	**Idadi**	**Taasisi**	**Idadi**
Vijiji		***Vijiji***	
Msisimo	3	Mavumba	4
Ligunga	3	Misyaje	3
Lusewa	5	Molandi	3
Amani	4	Mbatamila	3
Matepwende	3	Nampungu	1
Milonji	3		
Magazini	4		
Likusanguse	3		
	28		**14**
Kata		***Kata***	
Lusewa	2	Mavumba	2
Magazini	2	Mampungu	2
	4		**4**
Tarafa		***Tarafa***	
Sasawala	1	Nalasi	1
		Nampungu	1
	1		**2**
Wilaya		***Wilaya***	
Ardhi	2	Maliasili	4
Mipango miji	1	Mipango miji	1
Kilimo	1	Ardhi	1
Mifugo	1	Maji	2
Maliasili	8	Mipango	1
Maji	2	Kilimo	2
Mipango	1		
Maendeleo ya jamii	1		
	17		**11**
JUMLA	**50**		**31**
JUMLA KUU		**81**	



Washiriki kujiandikisha

Sala ya ufunguzi na kujitambulisha

Kabla ya kujitambulisha Dr Lerise aliwaomba wajumbe wachague mjumbe mmoja atakayeongoza sala ya ufunguzi. Kufuatia uchaguzi wa wajumbe Mr. Dickson Koishwa aliwaongoza wajumbe kufanya sala ya ufunguzi kwa kuomba mafunzo yaende salama, yawe na mafanikio, wajumbe na wawezeshaji wawe na afya njema na wafanye kazi iliyowaleta kwa ufanisi mkubwa. Sala ya ufunguzi ilifuatiwa na washiriki wa mafunzo kujitambulisha ambapo kila mshiriki alitambulisha jina lake, wadhifa wake na taasisi aliyotoka (**Angalia kiambatanisho Namba 2 na namba 3**).

Kuchagua mwenyekiti wa mafunzo

Dr Lerise aliwafahamisha wajumbe kwamba katika mafunzo kama haya ni muhimu kuchagua mwenyekiti wa mafunzo ambaye atakuwa ni kiungo kati ya washiriki na wakufunzi na kati ya washiriki wenyewe. Mwenyekiti huyo atakuwa pia na jukumu la kutoa matangazo na taarifa muhimu kwa washiriki, kupokea maoni, mapendekezo, malalamiko kuhusu mafunzo n.k. Kufuatia maelezo haya wajumbe walimchagua bwana Abbas Mangwala Katibu Tarafa wa tarafa ya Nalasi wilaya ya Tunduru, kuwa mwenyekiti wa mafunzo.

Hotuba ya ufunguzi na majadiliano

Mafunzo yalifunguliwa rasmi na bwana Ngomelo (Meneja wa mradi wa ushoroba wa Salous-Niassa) ambaye alisema kuwa lengo la mafunzo ni kuwapa washiriki ufahamu juu ya umuhimu wa kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi. Akaongezea kwa kusema kuwa mafunzo haya ni muendelezo wa shughuli za mradi wa ushoroba za kujenga uwezo wa wananchi na wadau wengine ili waweze kusimamia vizuri rasilimali zao kwa lengo la kuongeza tija katika shughuli za maendeleo.

Meneja mradi alisema kuwa watu hupata mafunzo juu ya uhifadhi na usimamizi wa maliasili aidha vijijini na vyuoni au kwa ziara za mafunzo. Kwa wanachi wa wilaya za Tunduru na Namtumbo, baadhi ya walimu walio mbele yetu walipita kila kijiji kufundisha sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na sheria ya ardhi ya kijiji ya mwaka 1999. Aliongezea kwa kusema kuwa baadhi ya washiriki wa mafunzo walipata nafasi ya kufanya ziara ya mafunzo iliyofanyika kuanzia tarehe 14 – 24/10/2007 kwa kutembelea mikoa mitano ya Tanzania ambayo ina miradi ya ushoroba.

Akiendelea Meneja mradi aliwafahamisha washiriki wa mafunzo kuwa tafiti nyingi za kutambua rasilimali na hali zake zimefanyika. (mfano utafiti wa mimea, utafiti wa mto Ruvuma, mapito au njia za biashara kati ya Msumbiji na Tanzania, misingi ya maisha na uchumi na utafiti wa kuidadi wanyamapori kwa kutumia ndege). Aliwafahamisha wajumbe kuwa tafiti na kazi zote zilizofanyika na zinazoendelea kufanyika zina lengo kuu moja ambalo ni kuhakikisha mradi wa Ushoroba wa Wanyamapori wa Selous-Niassa unahifadhiwa kikamilifu kwa kuanzisha mtandao wa Maeneno ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (Wildlife Management Areas). Maeneo hayo yatalindwa, kusimamiwa na kutumiwa kiendelevu na jamii kwa msaada wa Halmashauri za wilaya za Namtumbo na Tunduru na Idara ya Wanyamapori.

Meneja aliwaeleza washiriki kuwa mafunzo watakayohudhuria yana lengo la kuwaandaa ili waweze kushiriki vizuri katika kazi ya kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ndani ya vijiji husika, ambao ndiyo muongozo wa kuwezesha kutenga maeneo kwa matumizi mbalimbali (kama kilimo, ufugaji, misitu ya hifadhi, hifadhi ya wanayamapori n.k) ambayo itafanyika kuanzia mwezi wa tano mwaka 2008. Ili kufanikisha zeoezi hili ni muhimu tuhakikishe kuwa hakuna migogoro ya mipaka kati ya vijiji vyetu.

Akimalizia alisema kuwa sisi sote ni wadau wa kuwezesha mpango huo kupatikana na akawaomba washiriki kusikiliza mafunzo kwa makini, kushiriki kila zoezi litakalotolewa na kutosita kuuliza pale ambapo hawataelewa ili watakapoondoka wawe walimu wa kwenda kuwaelimisha wale ambao hawakupata nafasi ya kuhudhuria mafunzo.

Ufunguzi wa mafunzo

Majadiliano

Baada ya ufunguzi Dr Lerise aliwaongoza washiriki kujadili walichokiona na/au kujifunza katika safari ya mafunzo. Washiriki walitaja mambo mengi waliyoona na kujifunza katika ziara yao. Miongoni mwa mambo hayo ni haya yafuatayo:

1. Ushiriki wa jamii ni muhimu sana katika uhifadhi
2. Mapato yanakuwa makubwa baada ya kuanzisha hifadhi
3. Mchakato wa uanzishaji maeneo ya hifadhi (WMAs) ni mgumu na unahitaji maandalizi mazuri na uvumilivu
4. Ni vizuri kutengeneza mazingira mazuri ya utekelezaji wa miradi ya maeneo ya jamii
5. Kwa kuwa na maji na uoto mazingira ya wilaya za Namtumbo na Tunduru mazuri zaidi kwa uhifadhi kuliko maeneo yaliyotembelewa na washirki
6. Maeneo ya hifadhi ni vituo vya kuvutia watalii (mfano ufugaji wa Nyoka Iringa). Vituo hivyo vinatunzwa vizuri sana.
7. Ili maeneo ya hifadhi yatengwe kwa ufanisi serikali za vijiji zishirikiane na jamii kwa kiasi kikubwa (ushirikishwaji uwe mkubwa sana)
8. Wanyama walio katika ushoroba katika maeneo yaliyotembelewa walionekana kuwa na hali nzuri kuliko wale wa maeneo ya washiriki
9. Maeneo mbali mbali yalionekana kuwa yametengwa kwa shughuli mbali mbali za uzalisahji na maendeleo
10. Uhifadhi umepunguza shida za kina mama kwa kutenga maeneo maalum ya kuni, kilimo, ufugaji n.k. Kina mama wengi walionekana kuwa mbele katika shighuli za ushoroba.
11. Uhifadhi unaweza kutumika kama njia ya kuzuia uharibifu wa wanyama kwa kutumia mbinu endelevu
12. Matumizi ya ardhi yamepangwa kijumuiya na hivyo kuna ushindani mkubwa wa matumizi mbali mbali ya ardhi
13. Kuna wana jamii waliopata ajira kutokana na kuanzishwa kwa miradi ya uhifadhi na hivyo wanapata kipato

Washiriki wa mafunzo juu ya mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi

Kwa ujumla majadiliano yalionesha kuwa wajumbe wengi wa ziara ya mafunzo hawajatoa marejesho ya ziara yao kwa jamii, jambo ambalo linawafanya wananchi wengi kutojua walichojifunza. Washiriki walishauri wajumbe wafanye marejesho kwa jamii mara tu watakapo rudi katika maeneo yao kutoka katika mafunzo haya. Walishauri pia ziara zaidi za mafunzo zipangwe kwa wengine ili mafunzo yapatikane kwa watu wengi kwa kujionea wenyewe.

Mradi wa ushoroba katika SADCC na InWent

Akitoa maelezo ya utangulizi Dr Lerise aliwafahamisha washiriki kuwa mradi wa ushoroba ni sehemu ya mradi mkubwa wa kimataifa unaohusisha nchi yetu na nchi jirani ya Msumbiji. Eneo la ushoroba lipo katika eneo la mto Ruvuma ambalo usimamizi wake uko chini ya Tanzania na Msumbiji.

Akiendelea alisema InWent ambayo ni shirika la kujenga uwezo la serikali ya kijerumani linajihusisha na usimamizi wa eneo la mto Ruvuma katika masuala ya maji, misitu na mazingira. Jumuiya ya maendeleo ya nchi za kusini mwa Afrika (SADC) nayo pia inajihusisha na usimamizi wa eneo la mto Ruvuma katika msuala yanayohusu ardhi, misitu na wanyamapori. Kwa kuwa eneo la mradi wa ushoroba lipo katika eneo la mto Ruvuma basi InWent na SADC nazo zinajihusisha na mradi wa ushoroba. InWent kwa upande wake inashirikiana na SADC katika kusimamia mto Ruvuma na inashirikiana na mradi wa ushoroba katika kujengea wananchi uwezo wa kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi na mipango ya maendeleo.

Akimalizia Dr Lerise alisema kuwa mafunzo haya yatawaongezea washiriki uwezo katika kushirikiana na wenzao wa msumbiji. Aliwaomba wajione kuwa wanashiriki katika suala la kitaifa na kimataifa na hivyo wajifunze kwa juhudi kubwa ili kile watakachojifunza kiwe na manufaa kwa vijiji vyao, wilaya, nchi na eneo zima la kusini mwa Tanzania pamoja na nchi jirani ya Msumbiji.

Video ya Mto Ruvuma

Washiriki walioneshwa video ya utafiti uliofanyika katika mto Ruvuma ili waone matokeo halisi ya matumizi ya rasilimali yaliyopatikana katika utafiti huo. Baada ya kuangalia video hiyo washiriki walitaja mambo yafuatayo kuwa ni mafunzo waliyopata:

1. Mto Ruvuma ni rasilimali ya kimataifa, ni jinsi gani tunaweza kushirikiana na wenzetu katika matumizi yakeili tufanye matumizi endelevu
2. Zina zilizotumiwa na wanajamii katika shughuli zao za uzalishaji mali ni hafifu na wanajamii wanaonekana kuwa na vipato vya chini huku baadhi yao wakishiriki katika matumizi/biashara ya dawa haramu. Miradi ya uhifadhi inaweza kupunguza matatizo haya
3. Katika eneo la mto Ruvuma kuna rasilimali muhimu ambazo zinaweza kutumika kwa shughuli ya utalii na kukuza kipato cha jamii
4. Kuna haja ya kuandaa mpango wa kusimamia rasilimali zilizopo
5. Uvunaji wa rasilimali (mf. madini na uvuvi) siyo endelevu.
6. Kuna kila sababu ya kushirikishaji jamii katika mipango ya maendeleo na hasa katika miradi ya uhifadhi
7. Jamii inapaswa kupata elimu ambayo itatumika katika kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi

1.2 Matarajio ya washiriki

Lengo

Kuweka kipimo cha kufanyia tathmini kwa mshiriki binafsi na wakufunzi ili kuona ni kwa kiasi gani mshiriki amepata kile alichotarajia kutoka katika mafunzo

Utangulizi

Washiriki waligawanywa katika makundi manne kutokana na taasisi zilizowakilishwa katika mafunzo. Kila kundi liliwasilisha matarajio kwa mujibu wa taasisi yao/zao. Kwa ujumla makundi yalikuwa matano pamoja na kundi la kina mama. Makundi hayo ni *washiriki ngazi ya vijiji (wilaya ya Tunduru), washiriki ngazi ya vijiji (wilaya ya Namtumbo), washiriki ngazi ya kata (zote) pamoja na madiwani, washiriki ngazi ya wilaya (zote) pamoja na madiwani, na washiriki wanawake (kina mama).*

Mbinu za kujifunza

i. Kutengeneza vikundi kazi
ii. Kujadili katika vikundi kazi
iii. Mawasilisho kwa vikundi
iv. Majadiliano

Mawasilisho na majadiliano

Kundi la kwanza: Washiriki ngazi ya vijiji (wilaya ya Tunduru)

Watendaji na viongozi katika ngazi ya vijiji kwa wilaya ya Tunduru walitarajia yafuatayo kutoka katika mafunzo;

i. Kupata elimu kuhusu mpango wa matumizi bora ya ardhi
ii. Kupata elimu na ujuzi wa kupima vijiji na kupata hati miliki ya ardhi ya kijiji
iii. Kupata elimu juu ya matumizi bora ya ardhi ambayo itawawezesha kuwa na uwezo wa kuwaelimisha wananchi mambo mbali mbali yanayohusu matumizi bora ya ardhi
iv. Kupata elimu itakayowewezesha kutatua migogoro ya ardhi kati ya kijiji na kijiji
v. Kuweza kutenga maeneo (km eneo la uhifadhi, kilimo, ufugaji, na makazi) na hivyo kukamilisha ushoroba
vi. Kupata uwezo mkubwa wa kushirikiana na wataalamu ngazi ya wilaya, tarafa, na kata.
vii. Kupata elimu ya utunzaji wa vianzo vya maji kwa kutunza misitu na maliasili zote kwa ujumla

Kundi la pili: Washiriki ngazi ya vijiji (wilaya ya Namtumbo)

Watendaji na viongozi katika ngazi ya vijiji kwa wilaya ya Namtumbo walitarajia kupata yafuatayo:

i. Kupata elimu ya uhifadhi wa maliasili zilizopo (kijijini)
ii. Kufahamu maana ya uhifadhi wa ardhi (uhifadhi wa radhi ni nini?)
iii. Kutambua matatizo ya ardhi na ufumbuzi wake
iv. Kupata elimu/utaalamu kuhusu upimaji wa ardhi ya kijiji na kuweka mipaka yake
v. Kujenga ushirikiano kati ya kijiji na kijiji kwa washiriki kujuana
vi. Kupata elimu kuhusu mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi
vii. Kupata maelekezo ya jinsi ya kupata cheti cha miliki ya ardhi ya kijiji
viii. Kupata elimu na mbinu za kuifikishia jamii kile walichojifunza

Kundi la tatu: Washiriki ngazi ya kata pamoja na madiwani

Yafuatayo yalikuwa matarajio ya washiriki ngazi ya kata:

i. Kuongeza uelewa wa uhifadhi wa maliasili na rasilimali nyingine (kama kuelewa mchakato wa uandaaji mipango ya matumizi bora ya ardhi, maliasili n.k.)
ii. Kupata mbinu za kuwawezesha washiriki kurudisha elimu watakayopata kwa jamii (vijijini)
iii. Kufahamiana na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya uhifadhi wa maliasili na rasilimali nyingine
iv. Kupata posho ya kujikimu

Kundi la nne: Washiriki ngazi ya wilaya pamoja na madiwani

Washiriki ngazi ya wilaya walitarajia mafunzo yatawapatia mambo yafuatayo:

i. Kupata njia na mbinu shirikishi za kuwawezesha kusitisha shughuli haramu zinazofanywa na wananchi (km uchimbaji madini kando ya mto Ruvuma, ukataji wa miti na uvuvi haramu)
ii. Kujifunza jinsi ya kushirikisha jamii katika kuandaa mipango ya matumizi ya rasilimali zilizopo katika maeneo yao na kuzisimamia kupitia mipango shirikishi
iii. Kupata uelewa juu ya dhana ya ushoroba na jinsi ya kutekeleza mipango ya ushoroba
iv. Kupata uelewa kuhusu kuhamasisha wananchi kuunda vikundi vya ushoroba katika maeneo mbali mbali kwa ngazi ya wilaya
v. Kufahamu hatua au taratibu za kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya rasilimali (km ardhi, madini, wanyamapori n.k) katika ngazi ya wilaya
vi. Kukutana, kufahamiana na kubadilishana uzoefu na washiriki wengine
vii. Kupata posho ya kujikimu

Kundi la tano: Washiriki wanawake (kina mama)

Kinamama walioshiriki mafunzo walitarajia yafuatayo kutoka katika mafunzo:

i. Kupata elimu ya matumizi bora ya ardhi, maliasili na rasilimali nyingine
ii. Kupanua uelewa wao kuhusu mchakato wa kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi
iii. Kupata uelewa na mbinu za kuwawezesha kuhamasisha jamii juu ya matumizi bora ya ardhi, maliasili na rasilimali nyingine
iv. Kufahamu jinsi ya kushirikisha jamii katika kuandaa mipango shirikishi na kusimamia rasilimali zilizopo
v. Kupata elimu itakayowawezesha kuhamasisha kina mama wagombee nafasi mbali mbali za uongozi ili yanapotokea mafunzo kama haya waweze kushiriki kwa asilimia mia moja
vi. Kupata posho ya kujikimu

1.3 Malengo na mbinu za mafunzo

Malengo

Malengo ya mafunzo yalikuwa:

i. Kuongeza uelewa wa wadau juu ya, sera, sheria, miongozo na dhana mbalimbali muhimu juu ya utunzaji na usimamizi wa maliasili
ii. Kubadilishana uzoefu juu ya kuandaa na kuteleza mipango shirikishi ya matumizi ya Ardhi katika ngazi ya Kijiji,
iii. Kuainisha majukumu na haki za wadau mbalimbali katika mchakato wa uandaaji wa mipanogo shirikishi ya Ardhi katika ngazi ya Kijiji,
iv. Kuwaandaa wadau kushiriki kikamilifu katika zoezi lijalo la kuandaa mipango shirikishi ya matumizi ya Ardhi kwa lengo la kufanikisha uanzishwaji wa eneo la hifadhi ya jamii (WMA)

Mbinu za mafunzo

Mbinu kuu za mafunzo zilizotumika zilikuwa:

i. Uwasilishaji wa mada (watoa mada/wawezeshaji)
ii. Maswali na majibu
iii. Washiriki kujisomea
iv. Kujadili kwa pamoja mifano hai
v. Kujadili katika Vikundi kazi na kuwasilisha
vi. Mazoezi kwa maigizo (Role play)
vii. Mazoezi kwa kutenda (Practical)

1.4 Sera mbali mbali na dhana ya ushirikishwaji

Lengo

Kufahamu maana halisi ya ushirikishwaji kama inavyoelezwa na sera ya maboresho, na kutathmini utekelezaji wake katika mipango halisi ya vijiji.

Utangulizi

Sera mbali mbali ziliangaliwa kwa kutumia mipango mbali mbali ya maendeleo na usimamizi wa ardhi iliyopo katika ngazi ya kijiji. Washiriki waliangalia jinsi dhana ya ushirikishwaji ilivyohusishwa katika utekelezaji wa mipango na changamoto mbali mbali za ushirikishwaji zilizojitokeza. Washiriki waligawanywa katika makundi manne yaliyotakiwa kujadili na kuwasilisha matokeo ya majadiliano yao kwa washiriki wote. Majadiliano yalitakiwa kujibu maswali matatu:

i. Mipango ya maendeleo na usimamizi wa ardhi na rasilimali asili (km ardhi, maji na misitu) katika ngazi ya kijiji inaandaliwaje?
ii. Sekta gani zinazoongozwa na utaratibu wa ushirikishwaji
iii. Kuna changamoto gani katika kutekeleza utaratibu wa ushirikishwaji katika ngazi ya kijiji, kata na wilaya?

Mbinu za kujifunza

i. Kutengeneza vikundi kazi
ii. Kujadili katika vikundi kazi
iii. Mawasilisho kwa vikundi
iv. Majadiliano na mawasilisho ya wawezeshaji

Mawasilisho na majadiliano

Vikundi vilifanya mawasilisho ya majadiliano yao kuhusu maswali matatu yaliyoulizwa. Mawasilisho hayo yalikuwa kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Namba 1.2 hapo chini. Katika majadiliano ulizuka mjadala juu ya maana halisi ya changamoto. Baadhi ya washiriki walifahamu changamoto kama fursa katika kutekeleza mipango ya maendeleo. Majadiliano ya wajumbe yakiongozwa na muwezeshaji (Dr Lerise) yalikubalian kuwa maana halisi ya changamoto ni kikwazo au msukumo katika kufanya au kutekeleza jambo.

Muwezeshaji (Dr Lerise) alifafanua pia dhana ya ushirikishwaji kwa kueleza aina za ushirikishwaji zinazofanywa na wadau mbalai mbali katika mipango ya maendeleo. Alitaja aina kuu tatu za ushirikishwaji:

a). Kutoa takwimu za kuandaa mpango

b) Kutekeleza mipango au miradi iliyoandaliwa na viongozi au wafadhili

b). Kushiriki katika kuibua vipau mbele, kuandaa mipango, kuchangia katika utekelezaji na kuratibu mafanikio (uwezeshaji)

Alimalizia kwa kusema kuwa maana halisi ya ushirikishwaji ni ile inayotambua umuhimu wa kutoa fursa ya kushiriki katika kufanya maamuzi na katika utekelezaji. Hivyo maana ya tatu ndiyo inayofaa zaidi kuwa maana ya ushirikishwaji kwa sababu:

i) Inawapa wananchi pamoja na viongozi wao fursa ya kutambua matatizo, kuweka vipau-mbele na kuibua mikakati ya utekelezaji wa pamoja. (Ushirikishwaji wa utekelezaji peke yake hautoshi)

ii) Inatoa fursa ya wadau kutoa maamuzi au kwa maneno mengine fursa ya kisiasa na ya kiutendaji.

Kwa vile serikali ya Tanzania inatambua umuhimu na mchango wa ushirikishwaji katika kupanua demokrasia na maendeleo endelevu, imetoa miongozo mbalimbali ya kuboresha ushiriki wa wananchi katika kupanga na kutekeleza miradi ihusuyo maendeleo yao. Miongoni mwa miongozo hiyo ni: *Maagizo ya Sera ya Maboresho (1998), maagizo ya Sera ya Ardhi, (1995), Maagizo ya Sera ya Mazingira (1992), Maagizo ya Sera ya Misitu, Maagizo ya Sera ya Wanyama Pori na Maagizo ya Sera ya Maji (2002)* **(**Angalia Hand out Namba 1 kwa maelezo zaidi**)**

Mawasilisho ya dhana ya ushirikishwaji

Jedwali Namba 1.2: Uandaaji wa mipango ya maendeleo vijijini, ushirikishwaji na changamoto zake

Jina la Kikundi	Matokeo ya majadiliano		
	Uandaaji wa mipango vijijini	**Sekta zinazoongozwa na ushirikishwaji**	**Changamoto za ushirikishwaji katika kuandaa mipango (kijiji, kata, na wilaya)**
Kundi Namba 1	Inaandaliwa na halmashauri ya kijiji, na kupitishwa na mkutano mkuu wa kijiji	i. Maji ii. Elimu iii. Afya iv. Kilimo/mifugo v. Maliasili	*Kijiji*: -Ugumu wa wananchi kuhudhuria mikutano *Kata*: -Usimamizi hafifu na ukosefu wa vitendea kazi *Wilaya*: -Ukosefu wa ufuatiliaji
Kundi Namba 2	Inaadaliwa kwa mbinu shirkishi inayowapa zinazowapa fursa wanavijiji wenyewe kuibua miradi na kushiriki katika utekelezaji wake mfano (O & OD)	i. Maliasili ii. Afya iii. Ardhi iv. Elimu v. Kilimo na mifugo vi. Maji	*Kijiji*: -Inachukua muda mrefu kufikia makubaliano -Rasilimali nyingi za fedha na watu zinahitajika *Kata*: -Kuna ukosefu wa wataalamu wa kutosha *Wilaya*: -Ufinyu wa bajeti ya kutekeleza miradi ya wananchi
Kundi Namba 3	Inaadaliwa kwa mbinu shirkishi (mf ardhi) na mingine si shirikishi (mf madini, utengaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii).	i. Ardhi ii. Misitu iii. Maji iv. Afya v. Elimu	*Kijiji*: -Uelewa mdogo wa wanakijiji -Kina mama wengi kutochangia hoja wakati wa kufanya maamuzi -Wanaume kutotoa nafasi kwa wanawake (mfumo dume) *Kata*: -Idadi ndogo ya wajumbe wanaoshiriki -Wenyeviti wengi ni wanaume, wanawake wananyimwa fursa ya kushiriki *Wilaya*: -Ushiriki mdogo wa kina mama katika ngazi ya uongozi na utendaji -Uelewa mdogo kwa baadhi ya wajumbe wa baraza la madiwani katika kutoa na kupitisha maamuzi
Kundi Namba 4	Inaandaliwa na makundi mbali mbali ya jamii (mf vijana, wazee, wanawake, makundi ya walemavu) kwa ushirkiano/usimamizi wa serikali ya kijiji	i. Ardhi ii. Kilimo iii. Elimu iv. Afya v. Maliasili vi. Maji vii. Mfuko wa Taifa wa kijiji (NSF)	

Majumuisho

Katika majumuisho ilionekana kuwa katika kupanga na kutekeleza mipango mbali mbali ya wanachi dhana ya ushirikishwaji ipo kinachotakiwa ni kuiboresha zaidi ili ichukue maana yake halisi. Ilionekana pia ushirikishwaji una changamoto mbali mbali ambazo nazo ni muhimu kuzifahamu na kuzifanyia kazi.

Ilionekana pia matarajio ya washiriki yaliendana na malengo ya mafunzo (angalia kipengele Namba 1.3). Hivyo washiriki walipata kile walichokitarajia. Yale yaliyokuwa nje ya uwezo wa wakufunzi yanatarajiwa kufanywa na ngazi husika, lakini kwa ujumla matarajio takriban yote yalifikiwa. Tathmini ya mafunzo iliyofanywa na washiriki wenyewe (**kiambatanisho Namba 4**) inaonesha kuwa kwa kiasi kikubwa matarajio yao yalifikiwa.

Mafunzo katika video ya mto Ruvuma yalionesha kuwa katika ushirikishwaji mawasiliano kati ya viongozi au watendaji na wanachi ni jambo la muhimu na yasipokuwapo mambo kama uharibifu wa rasilimali ulionekana katika mto Ruvuma yatatokea.

Mradi wa ushoroba ulifahamika kama suala la kimataifa linalohusisha wadau wa ndani na nje ya nchi. Hivyo ziara ya mafunzo katika miradi mingine ya ushoroba ilikuwa ya muhimu sana na ikapendekezwa kufanyika tena kwa wananchi wengine ambao hawakupata bahati ya kushiriki ziara iliyofanyika.

Rejea

Hand out Namba 1 – Sera mbali mbali na dhana ya ushirikishwaji.

SIKU YA PILI **JUMANNE 6/11/2007**

2.1 Uhusiano/uwiano mlalo wa mipango mbalimbali (horizontal integration)

Lengo

Kuwawezesha washiriki kutambua umuhimu wa mipango ya sekta mbali mbali kusaidiana ili kupata ufanisi katika mpango wa jumla

Utangulizi

Uhusiano/uwiano mlalo wa mipango ni ule uhusiano/uwiano unaotokea katika ngazi moja (mfano ngazi ya kijiji). Katika kujifunza mada hii washiriki waligawanywa katika makundi kwa kufuata vijiji vyao. Wilaya ya Namtumbo ilikuwa na vijiji 4 na Tunduru vijiji 2 jumla vijiji sita ambavyo vilifanya makundi 6. Kwa kuangalia hali ilivyo katika kijiji husika kila kundi lilitakiwa kujibu maswali yafuatayo:

Namtumbo

1. Katika mawasilisho ya siku ya kwanza, vijiji.vya Lusewa, Matepwende, Magazini na Likusanguse.vilitaarifu kuwepo kwa mipango shirikishi kadhaa. Mipango hiyo inawiana/husiana vipi?

Tunduru

2. Katika mawasilisho ya siku ya kwanza, vijiji.vya Molandi na Mbatamila.vilitaarifu kuwepo kwa mipango shirikishi kadhaa. Mipango hiyo inawiana/husiana vipi?

Mbinu za kujifunza

i. Kutengeneza vikundi kazi
ii Kujadili katika vikundi kazi
iii Mawasilisho kwa vikundi, maswali na majibu
iv Majadiliano

Mawasilisho na majadiliano

Baada ya majadiliano vikundi vyote vilifanya mawasilisho. Jedwali Namba 2.1 hapo chini linaonesha matokeo ya mawasilisho kutoka katika vikundi.

Jedwali Namba 2.1: Uhusiano/uwiano mlalo wa mipango

Wilaya	Kijiji	Miradi/mipango iliyopo	Uwiano/uhusiano
Namtumbo	Likusanguse	i. Elimu i. Maji ii. Afya iii. Maliasili (uhifadhi)	*Elimu na maliasili* Uchomaji wa tofali za kujengea madarasa unategemea kuni za miti ya kupanda kama miembe, na mikorosho iliyozeeka Eneo maalum la kukata miti ya kupasua mbao za kuezekea madarasa limetengwa *Elimu na maji* Ufyatuaji tofali za madarasa unategemea maji kutoka mradi wa kisima cha mdundiko wa kijiji
	Magazini	ii. Elimu - ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa i. Maji – uchimbaji wa visima kumi vya pampu ii. Afya – ujenzi wa nyumba ya mganga iii. Biashara – ujenzi wa soko la mazao na samaki iv. Kilimo/mifugo – mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe v. Maliasili – uhifadhi wa maliasili (samaki, nyuki, vyanzo vya maji)	Uhusiano/uwiano katika mipango upo lakini haujitokezi moja kwa moja.
	Lusewa	iii. Visima vinane vya maji (pampu) i. Mradi wa soko ii. Mradi wa ufugaji ng'ombe wa maziwa iii. Mradi wa kilimo cha umwagiliaji iv. Ujenzi wa madarasa v. Uhifadhi maliasili (ushoroba)	*Maji na afya* Upatikanaji wa maji safi na salama unapunguza milipuko ya magonjwa kama kuhara na kutapika na hivyo sekta ya afya haitumii kiasi kikubwa cha dawa *Maji na kilimo/mifugo* -Miradi ya maji hutoa maji ya kunyweshea mifugo -Upatikanaji wa maji kirahisi hufanya muda wa kazi za kilimo usipotee katika kutafuta maji *Maji, Kilimo na Biashara* Kilimo cha umwagiliaji hupata maji toka mradi wa maji, na mazao ya kilimo huuzwa sokoni na hutozwa ushuru hivyo kuendeleza soko.

	Matepwende	i. Maji – mradi wa TASAF ii. Afya – ukarabati wa zahanati iii. Elimu – ujenzi wa nyumba ya mwalimu iv. Jamii – benki tofali v. Ujenzi – mradi wa barabara (Lusewa-Matepwende) vi. Maliasili – mradi wa ushoroba	*Maji, afya ujenzi* Mradi wa TASAF unasaidia ujenzi wa huduma za jamii kama dispensari na zahanati *Maliasili, ardhi, kilimo/mifugo* Mipaka ya eneo la ushoroba inaandaliwa, mpango wa matumizi bora ya ardhi inabidi uandaliwe ili ushoroba uwepo rasmi
Tunduru	Molandi	iv. Utunzaji vyanzo vya maji v. Ujenzi wa visima 10 vi. Ujenzi wa madarasa 7 vii. Ujenzi wa nyumba za walimu 7 viii. Ujenzi wa ofisi ya kijiji ix. Ukarabati wa ghala la mazao x. Ukarabati wa josho xi. Ujenzi wa soko xii. Ujenzi wa skimu ya umwagiliaji xiii. Mpango wa matumizi bora ya ardhi	Uwiano/uhusiano haujitokezi moja kwa moja – tathmini ndogo ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa inaonesha: -Kuna upungufu wa madarasa manane -Kuna upungufu wa visima vinne
	Mbatamila	xiv. Kilimo i. Maliasili ii. Mpango wa matumizi bora ya ardhi iii. Ujenzi wa ofisi ya kijiji	*Kilimo na maliasilii* Inahusiana katika kupanga na kutambua mipaka ya maeneo ya kilimo na hifadhi *Kilimo na mpango wa matumizi bora ya ardhii* Mpango wa matumizi ya ardhi unatenga maeneo ya kilimo *Ujenzi wa ofisi na mpango wa matumizi bora ya ardhii* Mpango wa matumizi ya ardhi unabainisha na kutenga eneo zuri la ujenzi wa ofisi kwa kuzingatia mahitaji

2.2 Uhusiano/uwiano ngazi wa mipango mbalimbali (vertical integration)

Lengo

Kuwawezesha washiriki kutambua kuwa upangaji na utekelezaji wa mipango katika ngazi mbali mbali unahitaji kuhusisha ngazi nyingine za kiutawala na utekelezaji

Utangulizi

Uhusiano/uwiano ngazi wa mipango ni ule uhusiano/uwiano unaotokea katika ngazi tofauti za utawala na utendaji (mfano kijiji, kata na wilaya). Katika kujifunza mada hii vikundi 6 vilivyoelezwa mwanzoni viliendelea kujadili mada hii. Maswali yaliyotakiwa kujibiwa ni:

Namtumbo

1. Katika mawasilisho ya siku ya kwanza, vijiji.vya Lusewa, Matepwende, Magazini na Likusanguse.vilitaarifu kuwepo kwa mipango shirikishi kadhaa. Mipango hiyo inawiana/husiana vipi na mipango ya ***kata***?
2. Katika mawasilisho ya siku ya kwanza, vijiji.vya Lusewa, Matepwende, Magazini na Likusanguse.vilitaarifu kuwapo kwa mipango shirikishi. Mipango hiyo inawiana/husiana vipi na mipango ya ***wilaya ya.Namtumbo***.?

Tunduru

1 Katika mawasilisho ya siku ya kwanza, vijiji.vya Molandi na Mbatamila vilitaarifu kuwepo kwa mipango shirikishi kadhaa. Mipango hiyo inawiana/husiana vipi na mipango ya ***kata****?*
2 Katika mawasilisho ya siku ya kwanza, viijiji vya Molandi na Mbatamila.vilitaarifu kuwapo kwa mipango shirikishi kadhaa. Mipango hiyo inawiana/husiana vipi na mipango ya ***wilaya ya.Tunduru?***

Mbinu za kujifunza

i. Kutengeneza vikundi kazi
ii Kujadili katika vikundi kazi
iii Mawasilisho kwa vikundi, maswali na majibu
iv Majadiliano

Mawasilisho na majadiliano

Vikundi vyote vilifanya majadiliano na kuwasilisha matokeo ya majadiliano yao kwa washiriki wengine. Mawasilisho ya vikundi vyote ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Namba 2.2 hapo chini.

Rejea

Hand out Namba 2 – Mchakato wa kuandaa Mpango wa Maendeleo wa kijiji

Jedwali Namba 2.2: Uhusiano/uwiano ngazi wa mipango

Wilaya	Kijiji	Uhusiano/uwiano ngazi ya kata	Uhusiano/uwiano ngazi ya wilaya
Namtumbo	Likusanguse	Wananchi vijijini huandaa mipango na kuibua miradi ambayo hupelekwa kwenye kamati ya maendeleo ya kata (WDC) kwa kujadiliwa kuwianishwa na kupitishwa.	-Baraza la madiwani hupokea mipango ya kata na kuichambua kwa kuangalia vipaumbele vya taifa na wilaya. -Hurudishwa kwa wanachi vijijini vipau mbele vilivyochaguliwa kwa utekelezaji
	Magazini	-Kijiji huandaa mipango, kuibua miradi kuipeleka katika kikao cha maendeleo cha kata (WDC) -Kata hupokea mipango ya vijiji kuipitia na kufanya maboresho na hatimae kupeleka wilayani (katika baraza la madiwani)	Wilaya hupitia mipango na miradi iliyoainishwa katika kata zote na kurudisha mshindo nyuma kwa miradi iliyopitishwa au kurudishwa.
	Lusewa	Mipango inakwenda kwa ngazi mfano Elimu: Ngazi ya kujiji kuna MEM (Mpamgo wa maendeleo ya elimu ya msingi), ngazi ya kata kuna MMES (mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari)	-Wilaya hupitisha mipango ya kata kwa utekelezaji -Wilaya hutoa fedha za kutekeleza mipango na miradi mfano ujenzi wa sekondari ngazi ya kata, uendelezaji miradi ya kilimo
	Matepwende	-Mipango ya vijiji hupitishwa na vikao vya maendeleo vya kata (WDC) -Kata husaidia usimamizi wa mipango na miradi na kutoa ushauri wa kitaalamu	-Wilaya hujadili, kurekebisha na kupitisha mipango na miradi iliyoibuliwa katika ngazi ya kata -Hutoa fedha, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi na mipango iliyopitishwa na kurudishwa kwa wananchi kwa utekelezaji
Tunduru	Molandi	-Kijiji huibua miradi kutoka katika mpango wa kijiji na kupeleka katani (WDC) kwa kuthibitishwa na kupitishwa. -Kata huwianisha mipango ya vijiji, kutoa ushauri na kupeleka mpango wa kata wilayani. -Kata hufanya ufuatiliaji na usimamizi	-Halmashauri ya wilaya hupitisha mipango na kuiwezesha ili iweze kutekelezwa -Halmashauri ya wilaya hufuatilia na kusimamia utekelezaji wa mipango
	Mbatamila	Mipango ya kijiji hupelekwa kwenye baraza la maendeleo la kata (WDC) ili kujadiliwa, kuthibitishwa na kuwianishwa na mipango ya vijiji vingine	Mipango ya kata hupelekwa kwenye baraza la madiwani kujadiliwa, kuthibitishwa na kuwianishwa na mipango ya kata nyingine ili kufanya mpango wa wilaya

2.3 Muundo wa kisheria na kitaasisi

Lengo

Kuongeza uelewa wa maelekezo ya sheria ya ardhi juu ya kuandaa na kutekeleza mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi

Utangulizi

Washiriki walifahamishwa taasisi mbali mbali ambazo zina nguvu ya kisheria katika kuandaa na kutekeleza mipango. Vifungu mbali mbali vinavyowapa wananchi nguvu ya kutayarisha mipango yao kwa usimamizi wa serikali za vijiji vilifafanuliwa.

Mbinu za kujifunza

i. Mawasilisho
ii. Maswali na majibu
iii. Majumuisho

Mawasilisho na majadiliano

Muwezeshaji (Dr Lerise) aliwafahamisha washiriki kuwa mipango shirikishi inaweza kutayarishwa kwa kutumia :

i. Sheria ya ardhi ya vijiji Namba 5 ya mwaka 1999
ii. Sheria ya matumizi ya ardhi Namba 6 ya mwaka 2007
iii. Miongozo ya ushirikishwaji katika mipango na usimamizi wa matumizi bora ya ardhi

Alizitaja aina mbali mbali za ardhi ambazo zinatambulika kisheria na ambazo zinaweza kutumika katika kufanya mipango mbali mbali ya matumizi ya ardhi. Aina hizo ni kama zifuatazo:

i. *Ardhi ya umma* - Ardhi yote nchini Tanzania
ii. *Ardhi ya jumla* – Ardhi yote ya umma ambayo siyo ardhi ya hifadhi au ardhi ya kijiji
iii. *Ardhi iliyohifadhiwa* – Ardhi iliyotengwa kama hifadhi ya misitu, mbuga za taifa za wanyama pori na maeneo mengine ya hifadhi na miji
iv. *Ardhi ya kijiji* – Ardhi ya umma ambayo mipaka yake imewekwa kwa sheria au utaratibu wa kiutawala kama ardhi ya kijiji

Muwezeshaji alisema kijiji kinasajiliwa kwa mujibu wa sheria Namba 7 ya mwaka 1982 ya serikali za mitaa na baada ya kutambua mipaka yake kinapata cheti cha ardhi ya kijiji. Cheti cha ardhi ya kijiji kinaipa serikali ya kijiji mamlaka ya kusimamia mipango ya kijiji kwa kutumia Halmashauri ya kijiji kama msimamizi mkuu. Kwa mujibu wa sheria Namba 6 ya mwaka 2007 cheti kinaipa Halmashauri ya kijiji uwezo wa kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji. Kama kuna rasilimali ya pamoja kwa vijiji viwili au zaidi kifungu cha 11 cha sheria Namba 6 ya mwaka 2007 kinatoa nafasi ya kuandaa mpango wa pamoja kwa vijiji husika.

Akimalizia Dr Lerise alisema kuwa baada ya kupata cheti cha ardhi ya kijiji sheria Namba 5 ya mwaka 1999 inatoa mamlaka kwa Halmashauri ya kijiji:

i. Kusimamia ardhi ya kijiji kwa mujibu wa sheria za mila husika
ii. Kulinda mazingira
iii. Kulinda haki za njia
iv. Kulinda na kutunza mipaka ya kijiji

v. Kutoa taarifa kwa kamishina wa srdhi kama mipaka imebadilika
vi. Kutoa hati ya haki miliki ya kimila
vii. Kutunza takwimu mbali mbali

2.4 Hatua za kuandaa Mpango shirikishi

Lengo

i. Kutambulisha na kuongeza ufahamu wa washiriki juu ya hatua za kuandaa mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi
ii. Kutambulisha na kuongeza ufahamu wa wahiriki juu ya kuundwa na majukumu ya kamati ya kijiji ya usimamizi wa matumizi ya ardhi (VLUM)

Utangulizi

Katika mada hii washiriki waligawanywa katika makundi 6 yenye vikundi 4 kwa Wilaya ya Namtumbo na vijiji 2 kwa wilaya ya Tunduru. Kila kundi/kijiji kilitakiwa kujibu maswali yafuatayo:

Namtumbo

1. Jadili hatua zilizofuatwa katika kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi wa kijiji cha
   i. Lusewa,
   ii. Matepwende
   iii. Magazini
   iv. Likusanguse

Tunduru

2. Jadili hatua zilizofuatwa katika kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji cha
   i. Molandi
   ii. Mbatamila

Washiriki walitakiwa pia kuzingatia yafuatayo:

i. Kitu gani kiliwasukuma kuandaa mpango?
ii. Mchango wa wanakijiji ulikuwa upi?
iii. Wilaya ilihusika vipi?
iv. Wataalamu gani walishiriki?
v. Ilichukua muda gani kukamilisha?
vi. Mpango huo unaonyesha nini?
vii. Mpango ulipitishwa na nani?
viii. Utekelezaji umefikia wapi?
ix. Utekelezaji unafanywa na nani?

Mbinu za kujifunza

i. Kuunda vikundi kazi
ii. Majadiliano katika vikundi
iii. Mawasilisho
iv. Maswali na majibu

Mawasilisho na majadiliano

Kila kundi ambalo lilikuwa linawakilisha kijiji husika liliwasilisha matokeo ya majadiliano yao kwa kujibu maswali yaliyoulizwa. Baada ya kuwasilisha washiriki waliuliza maswali ambayo yalijibiwa na wana kikundi huku muwezeshaji akisaidia kutoa ufafanuzi pale inapobidi. Matokeo ya mawasilisho ya kila kikundi ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Namba 2.3 hapo chini.

Rejea

Hand out Namba 3 – Mchakato wa kuandaa mpango shirikishi wa kijiji

Ramani ya kijiji kuonesha matumizi ya ardhi - Kijiji cha Magazini

Jedwali Namba 2.3: Hatua za kuandaa mpango shirikishi

Wilaya	Kijiji	Msukumo	Mchango wa wanakijiji	Wilaya ilivyohusika	Wataalam walioshiriki	Muda uliotumika	Mpango unaonesha nini	Taasisi iliyoupitisha	Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa	Mtekelezaji
Namtumbo	Lusewa	Kuepusha migogoro ya matumizi ya ardhi kwa wanakijiji	-Mawazo kupitia vikao halali -Kutoa maeneo yao ili kufanikisha mpango	Haikuhusika	Hakuna	Mwaka 1	Matumizi ya ardhi -Makazi -Kilimo -Ushoroba -Vyanzo vya maji -Malisho	Mkutano mkuu wa kijiji	Unaendelea	Halmashauri ya kijiji
	Matepwende	Ongezeko la idadi ya watu kulinganisha na mahitaji	-Hoja katika mikutano -Nguvu kazi -Fedha taslimu	Haikuhusika	Hakuna	Mwaka 1	Matumizi mbali mbali ya ardhi	Wanakijiji wenyewe	Kama inavyoonesha ramani	Wanakijiji wenyewe
	Magazini	-Ongezeko la idadi ya watu -Uharibifu wa mazingira na maliasili -Ongezeko la migogoro ya ardhi	-Kutoa maoni ya kuainisha matumizi bora ya ardhi -Kutoa nguvu kazi	Haikuhusika	Hakuna	Mwaka 1	Matumizi bora ya ardhi (tazama ramani)	Wananchi katika mkutano mkuu	Maeneo yaliyoainishwa yametengwa na yanatumika	Wananchi (jamii ya wana Magazini)
	Likusanguse	-Kuepusha migogoro ya matumizi ya ardhi -Kupunguza uharibifu wa rasilimali	Kutoa maoni na uamuzi	-Kukubali maoni ya wanakijiji -Kutoa wataalamu	Wataalamu wa -Kilimo -Maji -Mipango -Afya -Ardhi	Miezi mitatu 3	Matumizi bora ya ardhi	Mkutano mkuu wa kijiji	Maeneo yaliyobainishwa yanatumika kama ilivyopangwa (maeneo ya zahanati, shule, makaburi, michezo, ibada na makazi)	Wanakijiji wakiongozwa na Halmashauri ya kijiji
Tunduru	Molandi	-Kupunguza migongano ya mtumizi ya ardhi katika jamii -Kuongezeka kwa mahitaji muhimu ya jamii (km sehemu ya kuzikia, kilimo, shule)	Mchango wa mawazo kupitia mikutano	Ilitoa wataalamu	Wataalamu wa -Elimu -Maliasili -Kilimo -Mifugo -Mazingira	-Mwaka 1 (eneo la ushoroba na vianzo vya maji) -Maeneo mengine – tangu kijjij kianzishwe 1976	Matumizi mbali mbali ya ardhi -Kuzikia -Makazi -Ushoroba -Vyanzo vya maji -Shule -Malisho -Kilimo -Umwagiliaji -Josho	Mkutano mkuu wa kijiji	Maeneo mbali mbali yanatumika kama yalivyotengwa	Wanakijiji wakishirikiana na wataalamu ngazi ya kata
	Mbatamila	-Migogoro ya ardhi (kwa kilimo, malisho na ujenzi) -Ongezeko la watu (kuzaliwa na kuhamia) -Kuingia kwa mradi wa ushoroba	-Kutoa takwimu na taarifa za mazingira -Kujadili na kupitisha mpango	Kutoa wataalamu na rasilimali (vitendea kazi)	-Wataalamu wa ugani toka sekta mbali mbali pamoja na -Afisa mtendaji (kata) -Mratibu elimu (kata) -Mratibu elimu (wilaya)	Siku 9	Matumizi mbali mbali ya ardhi -Kilimo -Malisho -Hifadhi ya misitu	Ulipitishwa katika ngazi ya kata, ukapelekwa wilayani (Baraza la madiwani)	Haujatekelezwa – maeneo yake hayajapimwa	Mpango haujatekelezwa

Ramani zinazoonesha matumizi ya ardhi - Vijiji vya Molandi na Matepwende

2.5 Hatua za kupitisha na kutekeleza Mpango shirikishi

Lengo

Kutambulisha taasisi zinazohusika kisheria kupitisha na kutekeleza mpango

Utangulizi

Muwezeshaji (Dr Lerise) aliwasilisha mada ya mchakato au hatua za kupitisha mpango uliotayarishwa kwa utaratibu wa ushirikishwaji. Baada ya mawasilisho washiriki walipata nafasi ya kuuliza maswali na kupata ufafanuzi zaidi.

Mbinu za kujifunza

i. Mawasilisho
ii. Maswali na majibu

Mawasilisho na majadiliano

Akiendelea na mawasilisho ya mada Dr Lerise alitaja taasisi zinazohusika na kupitisha na kutekeleza mpango. Taasisi hizo na hatua au mchakato unaofuatwa ni kama inavyooneshwa hapo chini:

i. Kuwasilisha mpango kwenye mkutano mkuu wa kijiji ili uidhinishwe/upitishwe
ii. Waziri anayehusika na mipango ya matumizi bora ya ardhi atatangaza mpango katika eneo muafaka
iii. Mpango utawasilishwa wilayani ili ukahusishwe na mpango wa wilaya ikiwa ni pamoja na kufanyiwa marekebisho
iv. Mpango unaweza kusitishwa na Tume ya Taifa ya Matumizi bora ya ardhi kwa kutoa mapendekezo ya kusitisha mpango kwa waziri endapo kutakuwa na ugumu wa utekelezaji
v. Kama usitishwaji mpango haukufanyika utekelezaji utaendelea (kwa mfano ushoroba)

Rejea

Hand out Namba 3 – Kipengele Na 6

2.6 Wajibu na majukumu ya watendaji katika mipango shirikishi na usimamizi wake

Lengo

Kubainisha wadau mbali mbali katika mchakato wa kuandaa mipango shirikishi na kutambulisha majukumu yao

Utangulizi

Muwezeshaji (Dr Lerise) alitaja watendaji mbali mbali ambao ni wadau katika uandaaji mipango shirikishi na majukumu ya kila mdau (taasisi). Katika ngazi ya kijiji halmashauri ya kijiji ilionekana kuwa ndiyo yenye jukumu kubwa kutekeleza na kusimamia mpango shirikishi wa kijiji. Alibainisha wajibu na majukumu ya jumla kwa kila mmiliki wa ardhi kama ifuatavyo:

i. Kutekeleza matumizi ya ardhi ya eneo lake kama linavyooneshwa kwenye mpango wa kijiji bila kushurutishwa
ii. Kujua haki zake kwa eneo analomiliki na kuzilinda

iii. Kutoa taarifa na takwimu sahihi zinapohitajika
iv. Kushiriki kwenye maamuzi (mf. Mkutano wa kuwasilisha na kujadili mpango, mkutano mkuu wa kijiji wa kupitisha mpango)
v. Kuhamasisha wananchi wenzake

Mbinu za kujifunza

i. Mawasilisho
ii. Maswali na majibu

Mawasilisho

Katika kuwasilisha mada hii muwezeshaji (Dr Lerise) alibainisha wadau katika utekelezaji wa mpango wa kijiji na majukumu yao. Alisema wadau katika mchakato wa utekelezaji ni:

vi. Kamati ya usimamizi wa matumizi ya ardhi ya kijiji (VLUM)
vii. Wataalam wa ngazi za chini kijijini (village technicians)
viii. Halmashauri ya kijiji
ix. Mkutano mkuu wa kijiji
x. Mtendaji wa kijiji (VEO)
xi. Kamati ya maendeleo ya kata (WDC)
xii. Halmashauri ya wilaya (full council)
xiii. Sekretarieti ya mkoa
xiv. Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi
xv. Waziri anayehusika na mipango

Majukumu ya kila mdau yanaoneshwa katika hand out Na 4**.**

Rejea

Hand out Namba 4 – Majukumu ya wadau mbali mbali

2.7 Majumuisho

Katika majumuisho ya siku ya pili Dr Lerise aliwafahamisha wajumbe kuwa kwa mujibu wa sheria na miongozo mbali mbali (mfano sheria Na 6 ya 2007, sheria Na 7 ya 1982 na muongozo wa kuandaa mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi) hatua za kuandaa mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi ni hizi zifuatazo:

i. Halmashauri ya kijiji kutoa tamko la kusudio la kuandaa mpango (kif 25, sheria Na 6 ya 2007)
ii. Kutathmini rasilimali zilizopo
iii. Kuainisha ubora wa maeneo
iv. Kutambua mahitaji ya ardhi ya sasa na ya baadae
v. Kutenga maeneo kulingana na mahitaji ya viwango husika (kv kilimo, misitu, makazi, vyanzo vya maji, malisho, ushoraba n.k)

Kwa ujumla mawasilisho ya mada mbali mbali yaliyofanywa na washiriki pamoja na majadiliano yake yalioneshha mambo yafuatayo:

i. Ushirikishwaji ni mchakato mgumu unaohitaji uvumilivu na umakini katika utekelezaji wake

ii. Dhana ya uhusiano na uwiano wa mipango ipo katika hali halisi

iii. Kuunganisha mipango si sawa na kuwianisha hivyo kuna haja ya kuwianisha au kuhusianisha mipango (ili upatikane uhusiano au uwiano wa mipango) na wala si kuiunganisha

iv. Uwiano huimarishwa na ushirikishwaji na huwa unajitokeza wakati wa utekelezaji

v. Ardhi ni rasilimali mama ambayo karibu kila kitu kinaitegemea hivyo ni lazima ifanyiwe matumizi bora na endelevu

vi. Ardhi haiongezeki lakini mahitaji yetu yanaongezeka hivyo ni lazima tuwe na mipango ya matumizi bora ya ardhi

vii. Kuna umuhimu mkubwa wa kuhifadhi mazingira wakati wa kuandaa na kutekeleza mipango yetu

Mawasilisho ya makundi – Hatua za utayarishaji mpango

SIKU YA TATU **JUMATANO 7/11/2007**

3.1 Uhakiki wa rasilimali (Resource Assessment)

Lengo

Kuwawezesha washiriki kujua utaratibu wa kuandaa taarifa mbalimbali zinazohitajika ili kufanya maamuazi juu ya matumizi na utunzaji/usimamizi wa rasilimali

Utangulizi

Katika mada hii washiriki walifanya mafunzo kwa vitendo kwa kuhakiki rasilimali katika maeneo mawili yaliyopewa majina ya kijiji cha *uwiano* na *shirikisho.* Kabla ya kuanza zoezi hili washiriki na wakufunzi walikubaliana maana halisi ya rasilimali kuwa inahusisha vitu kama:

i. Wanyamapori
ii. Maji
iii. Misitu
iv. Ardhi
v. Madini
vi. Watu
vii. Miundo mbinu
viii. Maumbile ya kijiografia
ix. Hali ya hewa n.k.

Baada ya kufahamu maana ya rasilimali kila kijiji kilitengeneza makundi matano yenye watu wasiozidi 8. Kila kundi lilipewa kazi yake ya kutathmini kulingana na makundi ya rasilimali zilizoainishwa kama ifuatavyo:

Jedwali Namba 3.1: Mgawanyo wa makundi katika zoezi la kutathmini rasilimali

Na	Kundi la rasilimali ya kutathminiwa	Washiriki katika kundi	Maelezo ziada
1.	Maumbile ya kijiografia	Afisa mipango miji na vijiji na washiriki wengine wasiozidi 7	Kundi Na 1 kwa kila kijiji
2.	Aina za udongo na madini	Afisa kilimo/mifugo na washiriki wengine wasiozidi 7	Kundi Na 2 kwa kila kijiji
3.	Uoto wa asili na viumbe hai viishivyo katika eneo	Afisa misitu, maliasili, wanyamapori na washiriki wengine wasiozidi 7	Kundi Na 3 kwa kila kijiji
4.	Rasilimali za maji	Afisa maji na washiriki wengine wasiozidi 7	Kundi Na 4 kwa kila kijiji
5.	Matumizi ya ardhi na miundo mbinu iliyopo	Afisa ardhi, mipango miji na vijiji na washiriki wengine wasiozidi 7	Kundi Na 5 kwa kila kijiji

Washirki katika makundi walitakiwa kuzingatia mambo yafuatayo katika kufanya tathmini ya rasilimali:

i. Kuainisha rasilimali zilizopo kwa mujibu wa kazi katika kundi lao
ii. Kueleza sifa na umuhimu wa rasilimali husika (kijadi, kitaifa, kiuchumi, kiikolojia)
iii. Kuangalia na kurikodi hali ya rasilimali (status)
iv. Kuangalia matumizi ya sasa ya rasilimali

v. Kuangalia mabadiliko ya rasilimali (yanayotokana na hali ya hewa au shughuli za binaadamu)
vi. Kuangalia mambo yanayotishia ubora na uendelevu wa rasilimali
vii. Kuangalia vikwazo na fursa katika kutumia na kuendeleza rasilimali husika

Makundi yote kumi yalipatiwa usafiri wa kwenda katika eneo husika na kufanya tathmini ya rasilimali kwa vitendo na baadae kuwasilisha kwa washiriki wengine kama inavyooneshwa katika kipengele cha mawasilisho.

Mbinu za kujifunza

i. Kuunda vikundi kazi
ii. Kazi katika eneo husika (fieldwork)
iii. Mawasilisho na majadiliano

Mawasilisho na majadiliano

Makundi yote yalifanya mawasilisho ya tathmini ya rasilimali katika kundi la rasilimali husika. Washiriki wengine walipata nafasi ya kuuliza maswali na kupata ufafanuzi toka kwa wawasilishaji na wakufunzi. Matokeo ya uwasilishaji kwa kijiji cha Shirikisho (ambayo yametumika kama mfano) ni kama inavyooneshwa katika jedwali Namba 3.2 hapo chini.

Rejea

Hand out Namba 5 – Uhakiki/tathmini ya rasilimali kwa matumizi mbali mbali

3.2 Kutenga maeneo kwa matumizi mbali mbali (Resource use options)

Lengo

i. Kutenga maeneo kutokana na mahitaji ya jamii ya sasa na badae ili kuwezesha upangaji wa masharti ya matumizi au uendelezaji

ii. Kuoanisha matumizi na milki na kuandaa ramani ambayo baada ya kupitishwa itatoa mpango wa matumzi bora wa kijiji

Utangulizi

Makundi yaliyotengenezwa katika zoezi la kutathmini rasilimali yaliendelea kufanya kazi katika zoezi hili kama kundi moja la kijiji cha *Uwiano* au *Shirikisho*. Yalifanya kazi kwa pamoja kwa kuwianisha tathmini/uhakiki wa rasilimali zote na hatimae kutenga maeneo ya matumizi mbali mbali ya kijiji (kwa kuangalia ubora wa maeneo) ambayo yalifanya mpango wa matumizi bora ya ardhi wa kijiji. Pia washiriki waliandaa ramani kuonesha ubora wa eneo kwa matumizi mbali mbali, na hatimae ramani ya mpango wa matumizi bora ya ardhi wa kijiji.

Katika kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi washiriki walitakiwa kutumia taarifa muhimu za kijiji zifuatazo ambazo zilibuniwa ili kukamilisha zoezi hili:

Taarifa muhimu kuhusu eneo la mpango

1) Idadi ya watu katika kijiji iwe 320
2) Idadi ya kaya iwe 50
3) Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo, ufugaji, biashara na ajira mjini
4) Mila na desturi ni:
    i. Mchanganyiko wa makabila - 40%,
    ii. Wangoni - 60%,
    iii. Dini zilizopo: wakristu, waislamu na dini za asili
5) Eneo hilo ni ardhi ya kijiji
6) Hali ya hewa ni kama ya kijiji cha *Likusanguse* au *Molandi*

Mambo ya kuzingatia katika kutenga maeneo

i. Mpango uwe wa muda wa miaka 10
ii. Uzingatie mahitaji ya ardhi kwa shughuli mbalimbali
iii. Uzingatie hali halisi (existing situation)
iv. Uzingatie kukubaliana/kupatana kwa matumizi ya ardhi (land use compartibility)
v. Uzingatie uhifadhi wa mazingira na maeneo ya hifadhi (sensitive areas –maeneno nyeti, mf beach areas – maeneo ya pwani ya ziwa au bahari, swamps –maeneo yenye maji yaliyotuama/ardhi oevu, vyanzo vya maji n.k)
vi. Uzingatie matokeo ya tathmini ya rasilimali (resource assessment)
vii. Uzingatie kutenga maeneo ya uma (makaburi, shule, barabara n.k)
viii. Mapendekezo yawe kwenye ramani ya matumizi bora ya ardhi

Mbinu za kujifunza

iv. Vikundi kazi
v. Majadiliano katika vikundi
vi. Mawasilisho, maswali na majibu

Mawasilisho na majadiliano

Kila kijiji kiliwasilisha maeneo mbali mbali yaliyotengwa kutokana na tathmini ya rasilimali zilizopo na ubora wa maeneo kwa matumizi mbali mbali katika kijiji. Vijiji pia viliwasilisha ramani ya mpango wa matumizi bora wa kijiji ulioandaliwa kutokana na matumizi mbali mbali ya kijiji kama kilimo, malisho, maeneo ya vianzo vya maji, maeneo ya shule, serikali ya kijiji n.k. Mawasilisho ya kijiji cha Shirikisho yanaoneshwa katika Jedwali Namba 3.3.

Rejea

Hand out Namba 6 – Kutenga maeneo kwa matumizi mbali mbali ya rasilimali

Jedwali Namba 3.2: Uhakiki/tathmini ya rasilimali –Kijiji cha shirikisho

Kijiji	Kundi la rasilimali	Rasilimali zilizopo	Sifa na umuhimu wake	Hali yake (status)	Matumizi yake (ya sasa)	Mabadiliko ya rasilimali	Mambo yanayotishia ubora wake	Vikwazo na fursa katika kuziendeleza
Kijiji cha Shirikisho	Maumbile ya kijiografia	i. Eneo ni karibu tambarare ii. Bonde linalokatisha kijiji iii. Mabwawa ya kuchimbwa iv. Korongo v. Mtaro wa maji taka/ya mvua	i. Eneo ni karibu tambarare linafaa kwa maendeleo ya ujenzi, kilimo, mifugo na miundo mbinu ii. Bonde ni muhimu kwa bustani, samaki na chanzo cha maji iii. Mabwawa ni mazuri kwa ufugaji wa samaki, iv. Mtaro hudhibiti maji ya mvua	i. Eneo tambarare ni zuri halijaharibiwa ii. Mabwawa hayana maji wala samaki ii. Bonde karibu linakauka kutokana na matumizi mabaya v. Mtaro umejengwa kwa simenti	i. Eneo la tambarare limejengwa nyumba za makazi ii. Mtaro unapitisha maji ya mvua ii. Korongo linachimbwa mchanga kwa ajili ya ujenzi	Hakuna		
	Aina za udongo na madini	i. Udongo ii. Bonde lenye udongo chepe chepe iii. Madini (Hakuna)	i. Kokoto kwa ajili ya ujenzi zinapatikan ii. Udonga ni mzuri kwa kutengeneza tofali iii. Bonde linafaa kwa kilimo cha bustani na ufugaji wa samaki	i. Sehemu ya eneo halifai kwa kilimo ii. Sehemu ya eneo inafaa kwa kilimo	i. Utengenezaji wa tofali ii. Ufugaji wa samaki	i. Uharibifu wa mazingira kutokana na uchomaji tofali, uchimbaji kokoto	i. Shughuli za kibinadamu zinazoendelea km uchimbaji kokoto, ukataji miti	Vikwazo i. Uharibifu wa mazingira ii. Elimu ndogo juu ya matumizi mazuri ya rasilimali ardhi Fursa i. Uwezekano wa kilimo cha bustani ii. Uwezekano wa kufuga samaki iii. Upandaji miti katika eneo lililochimbwa kokoto
	Uoto wa asili na viumbe hai vilivyopo	Uoto (katika bonde) i. Nyasi fupi fupi na matete ii. Vichaka						

		iii. Miti (miyombo, michanga, miwanga, migunga, mifudu, mitanga) iv. Miti ya kupanda (miembe, miti ubani, mikaratusi, misendereo, minazi, mianzi) Viumbe hai i. Ng'ombe, mbuzi, kuku, bata, mbwa, paka, ndege, nyuki, vipepeo, panzi, mchwa, sisimizi, keren'gende						
	Rasilimali za maji	i. Mto ii. Mabwawa	i. Mto huwa na maji ya kutosha wakati wa masika ii. Mabwawa ni ya samaki na ni ya kuchimbwa na watu	i. Mto unakaribia kukauka kabisa ii. Mabwawa hayana maji	i. Kilimo kinafanyika ii. Malisho ya mifugo	i. Maji yamepungua kwa kiasi kikubwa kutokan na shughuli za kilimo na malisho ya mifugo	i. Migogoro ya ardhi ii. Migongano ya kisiasa	Fursa i. Kuwepo kwa mto ii. Sheria Na 5 na 6 za 1999 na 2007 Vikwazo i. Migogoro ya ardhi ii. Rasilimali fedha
	Matumizi ya ardhi na miundo mbinu iliyopo	i. Ardhi ii. Barabara iii. Maji iv. Majengo v. Watu	i. Barabara ya lami toka mjini songea ni muhimu kwa usafirishaji ii. Maji ni ya visima vya pampu hayatoshelezi mahitaji	i. Barabara toka ya lami toka Songea iko katika hali nzuri ii. Visima vya pampu vinafanya kazi iii. Sehemu kubwa ya ardhi imejengwa nyumba	i. Barabara inatumika kwa shughuli mbali mbali (usafiri wa abiria, mazao, nk) ii. Maji yanatumika kwa matumizi ya nyumbani (ispokuwa kunywa) ii. Majengo yanatumiwa kwa makazi na shughuli za dini			

Kijiji cha Shirikisho

Na	Maelezo muhimu	Idadi/Eneo
1.	Eneo la kijiji	Ekari 180
2.	Idadi ya watu (baada ya miaka 10)	Watu 800
3.	Idadi ya kaya	Kaya 64

Jedwali Namba 3.3: Maeneo yaliyotengwa kwa matumizi mbalia mbali (kijiji cha Shirikisho)

Namba	Matumizi	Eneo lililotengwa	Kigezo
1.	Eneo la kilimo	Ekari 64	i. Eneo la kijiji ni ndogo ii. Jamii itahamasishwa kutumia vizuri eneo hilo
2.	Eneo la mifugo Aina ya ufugaji ni ufugaji wa ndani Kila mwananchi ataruhusiwa kufiga wanyama wasiozidi ng'ombe 2, mbuzi 4, na nguruwe 4	Ekari 50	Eneo la ardhi ni dogo Idadi ya mifugo ni michache, ufugaji wa ndani unafaa zaidi kuliko ufugaji huria Sheria (ndogo za kijiji) zinakataza ufugaji holela
3.	Eneo la kuabudia Kuna madhehebu 5 Kila dhehebu ekari 1	Ekari 5	Eneo la kijiji ni dogo Kuna ongezeko dogo la waumini kulingana na ongezeko la idadi ya watu
4.	Taasisi (A) Shule	Ekari 12	Sera ya elimu inataka eneo la shule lisipungue ekari 12 Mahitaji ya elimu (shule) ni endelevu
	(B) Zahanati	Ekari 2	Udogo wa eneo la kijiji
5.	Makazi	Ekari 17	Udogo wa eneo la kijiji Kila mwanakijiji anahitaji eneo la makazi Kuna ongezeko dogo la idadi ya watu
6.	Maeneo ya makaburi • Waislamu ekari 1 • Wakristo ekari 1	Ekari 2	i. Udogo wa eneo la kijiji ii. Matukio machache ya vifo kutokana na huduma bora ya afya
7.	Maeneo ya burudani	Ekari 3	Burudani ni muhimu ili kujenga afya na akili Eneo la kijiji ni dogo
8.	Eneo la biashara	Ekari 5	i. Kukua kwa shughuli za kiuchumi ii. Kuongezeka kwa shughuli za minada
9.	Eneo la akiba	Ekari 20	i. Kijiji kina eneo dogo, eneo la akiba haliwezi kuwa kubwa ii. Kulingana na ongezeko la idadi ya watu kila kaya itaongezwa robo ekari baada ya miaka 10
Jumla		**Ekari 180**	

3.3 Majumuisho

Majumuisho ya siku ya tatu ya mafunzo yalifanywa na Dr Kideghesho ambaye alinukuu mambo muhimu yafuatayo kuwa ndiyo mafunzo makuu yaliyopatikana katika siku hii:

i. Kila kijiji kina mpango wa matumizi ya ardhi , mpango si lazima uwe ulitengenezwa na wataalamu hata unaotengenezwa na kutumika na wanakijiji katika shughuli za kila siku huo ni mpango
ii. Cheti cha ardhi ya kijiji ni muhimu sana kwa maendeleo ya kijiji. Bila cheti ruhusa ya kupanga mpango ambao utapitishwa na wizara haiwezi kutolewa
iii. Uandaaji wa mpango una hatua zake na ni muhimu zikafuatwa
iv. Halmashauri ya kijiji ina mamlaka na majukumu makubwa katika usimamizi wa ardhi ya kijiji

Dr Kideghesho aliainisha mambo muhimu (vigezo) vya kuangalia wakati wa kutathmini rasilimali kuwa viko katika makundi makubwa yafuatayo:

i. Vigezo vya kijamii (social criteria)
ii. Vigezo vya kiuchumi (economic criteria)
iii. Vigezo vya kisheria/kisera/kiasasi (legal/policy/institutional criteria)
iv. Vigezo vya kiikolojia/kimazingira (ecological/environmental criteria)

(Tazama hand out Namba 5 kwa maelezo ya kina)

Tathmini ya rasilimali – Mawasilisho ya makundi

SIKU YA NNE **ALHAMISI 8/11/2007**

4.1 Kuwasilisha mpango kwenye mkutano mkuu

Lengo

Kufahamu wadau na hatua zinazotakiwa kufuatwa katika kupitisha mpango ili utambulike kisheria

Utangulizi

Zoezi hili lilifanyika kwa vitendo katika makundi. Kulikuwa na makundi mawili yaliyowakilishwa na vijiji viwili (Uwiano na Shirikisho) katika kutathmini rasilimali, kutenga maeneo na kutayarisha mpango wa matumizi bora ya ardhi wa kijiji. Kila kijiji kilitengeneza makundi manane (8) ya wadau mbali mbali ambao walishiriki kutetea maslahi yao katika kupitisha mpango wa matumizi bora ya ardhi wa kijiji. Makundi hayo ya wadau yalikaa kama mkutano wa kijiji na kujadili mapendekezo ya mpango wa matumizi bora ya ardhi na kuupitisha baada ya kuridhika kuwa umezingatia mahitaji ya makundi yote muhimu. Makundi ya wadau na maslahi yao katika mkutano mkuu yanaoneshawa katika jedwali lifuatalo:

Jedawali Namba 4.1: Wahusika wa mkutano mkuu wa kijiji

Na	Wadau	Maslahi
1.	Mwenyekiti Mtendaji (VEO) Halmashauri ya kijiji	Kuhakikisha mpango unapita
2.	Kundi la kinamama	Kuona kwamba mpango umezingatia -Upatikanaji wa maji na nishati kwa njia rahisi kuliko hali ilvyo sasa -Ukaribu wa mashamba na makazi
3.	Kundi la vijana (wa kiume)	Kuona kwamba mpango umezingatia -Upatikanaji wa ajira -Upatikanaji wa ardhi ya makazi na shughuli za kiuchumi
4.	Kundi la wafugaji	Kuona kwamba mpango umezingatia -Upatikanaji wa eneo la malisho na maji -Eneo la malisho linakuwa mbali ya eneo la kilimo -Wanyama pori hawaleti athari kwa mifugo
5.	Kamati ya hifadhi	Kuona kwamba -Mpango unapitishwa
6.	Wakulima maarufu	Kuona kwamba mpango umezingatia -Upatikanaji wa ardhi ya kutosha ya kilimo -Wanyama pori hawaleti athari kwa mazao
7.	Kundi la walemavu	Kuona kwamba mpango umezingatia -Mahitaji ya walemavu -Meneo mbali mbali ya huduma muhimu yametengwa kwa viwango vinavyozingatia watu wenye ulemavu
8.	Kundi la wazee wa jadi	Kuona kwamba mpango umezingatia -Kuhifadhi maeneo ya matambiko -Kufikika kwa maeneo ya matambiko

Mbinu za kujifunza

i. Vikundi kazi
ii. Majadiliano (katik mkutano mkuu wa kijiji)
iii. Mawasilisho, maswali na majibu

Mawasilisho(Mkutano wenyewe)

Mkutano mkuu (katika vijij vyote viwili) uliendeshwa na mwenyekiti wa kijiji. Mtendaji wa kijiji alinakili majadiliano na kuandaa muhtasari wa mkutano, wajumbe wa halmashauri ya kijiji walisaidia kutoa majibu na ufafanuzi katika masuala mbali mbali yaliyoulizwa na wanakijiji. Mkutano ulikuwa na mvutano mkubwa kwa kuwa kila kundi lilikuwa linataka mahitaji yao yaonekane kwenye mpango. Mwishowe wajumbe waliupitisha mpango lakini kwa sharti kwamba ufanyiwe marekebisho yaliyopendekezwa na makundi mbali mbali ya wanakijiji.

4.2 Utekelezaji wa mpango

Lengo

Kufahamu mchakato wa utekelezaji wa mpango pamoja na mambo muhimu yanayotakiwa kuwapo ili mpango utekelezwe

Utangulizi

Wajumbe walijadiliana kuhusu maana ya kutekeleza mpango na kukubaliana kuwa kutekeleza mpango ni kuweka mapendekezo mbali mbali (yaliyopo kwenye mpango) katika uhalisia. Wanakijiji ni wadau muhimu katika utekelezaji wa mpango na wanatekeleza kama watu binafsi (mfano kulima katika eneo lilopangwa kwa kilimo, kuchunga katika eneo lilopangwa kwa malisho n.k). Pia wanatekeleza kwa kushiriki katika kuibua miradi ya jamii na kuitekeleza (mfano ujenzi wa shule, soko n.k). Mkufunzi (Dr Kideghesho) alielezea mambo muhimu yanayowezesha utekelezaji kuwa ni:

i. Kuhamasisha wadau kushiriki katika mchakato wa utekelezaji mpango (Na kufafanua jukumu la wadau katika mpango – yaani wadau watafanya nini)
ii. Kuibua miradi mbali mbali na kuitekeleza
iii. Kutunga sheria ndogo za kusimamia utekelezaji wa mambo yaliyomo katika mpango

Mbinu za kujifunza

i. Mawasilishoya wakufunzi
ii. Majadiliano
iii. Maswali na majibu

Mawasilisho na majadiliano

Washiriki wa makundi yote mawili walitengeneza makundi manane (8) ya wadau katika zoezi la utekelezaji wa mpango. Makundi hayo yalifanya zoezi la uibuaji wa miradi kama inavyoonesha katika kipengele cha kuibua miradi hapo chini.

4.3 Kuibua miradi kutoka mpango wa matumizi bora ya ardhi

Lengo

Kufahamu miradi mbali mbali inayoweza kuibuliwa kutoka katika mpango wa matumizi bora ya ardhi wa kijiji na kuandaa mikakati ya kuitekeleza

Utangulizi

Zoezi la kuibua miradi kutoka katika mpango wa kijiji lilitumia makundi tisa (9) ya wadau yaliyotengenezwa katika zoezi la kupitisha mradi katika mkutano mkuu. Kila kikundi kilitakiwa kuibua mradi na kuzingatia mambo yafuatayo katika mradi huo:

i. Aina ya mradi
ii. Msukumo wa kuanzisha mradi
iii. Malengo ya mradi
iv. Matunda yanayotegemewa kutokana na mradi
v. Taasisi zitakazojihusisha na mradi
vi. Rasilimali za mradi na vianzo vyake

Mbinu za kujifunza

i. Kuunda vikundi kazi
ii. Majadiliano katika vikundi
iii. Mawasilisho, maswali na majibu

Mawasilisho na majadiliano

Vikundi vyote viliwasilisha miradi iliyopendekezwa kwa kufuata vipengele sita vilivyoorodheshwa hapo juu. Washiriki wa kila kikundi walitakiwa kutetea mradi wao kwa kuelezea kwa nini rasilimali na muda utumike kutekeleza mradi huo. Washiriki wengine waliuliza maswali na kuomba ufafanuzi zaidi mahali ambapo hawakuelewa. Mawasilisho ya mradi wa kila kikundi ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Namba 4.2.

Mawasilisho ya kuibua miradi – Kundi la vijana

Jedwali Namba 4.2: Kuibua miradi kutoka kwenye mpango

Na	Kikundi	Aina ya mradi	Msukumo	Malengo ya mradi	Matunda ya mradi	Taasisi zitakazoutekeleza	Rasilimali na vianzo vyake
1.	Wazee wa jadi	Ufugaji wa mbuzi wa maziwa 12	Hali ngumu ya maisha i. Kutokana na umri kuwa mkubwa ufugaji wa mbuzi ni rahisi zaidi ii. Mbuzi wanazaana kwa muda mfupi (miezi 6) iii. Malisho yake ni rahisi kupatikana	i. Kupata kipato (pesa) baada ya kuuza maziwa ii. kupata maziwa ili kuboresha afya iii. Kupata nyama ili kujenga afya (kwa mbuzi watakaozeeka)	i. Maziwa ya kunywa na kuuza ii. Nyama ya kuuza na chakula iii. Ngozi kwa ajili ya kuuza (biashara)	i. Idara ya kilimo na mifugo ii. Idara ya maji iii. Idara ya ardhi na Maliasili (misitu)	i. Ardhi kwa ajili ya kuwatunza ii. Misitu kwa ajili ya malisho na zizi
2.	Walemavu	Ufugaji kuku wa kienyeji	i. Hali duni ya maisha (kipato kidogo) ii. Urahisi wa uendeshaji mradi iii. Matatizo ya kimaumbile (ulemavu)	i. Kufuga kuku 500 ii. Kuzalisha kuku 4500 iii. Kuuza kuku 4000@2500 mapato yatakuwa 10,000,000/= iv. Mgao uwe Tsh 500,000/= kwa kila mwanakikundi v. Kupumguza ukali wa maisha kwa wanakikundi vi. Kuuza samadi ya kuku ili kuongeza kipato	i. Kupata fedha ii. Kupata lishe bora iii. Kuboresha maisha	i. Taasisi/mashirika ya fedha ii. Wahisani mbali mbali (mashirika ya dini, mashirika yasiyo ya kiserakali (NGOs), Sekta ya mifugo, Halmashauri ya kijiji)	i. Rasilimali -Fedha -Kuku -Mabanda ya kuku ii. Vianzo -Michangoya wanakikundi -Misaada ya wahisani (Taasisi za dini, NGOs) iii. Mikopo ya mashirika ya fedha km Benki
3.	Wakulima maarufu	Kilimo cha umwagiliaji (Zao la mpunga)	i. Kupunguza umasikini ii. Kuongeza upatikanaji wa chakula iii. Kutumia vizuri rasilimali za ardhi na maji zilizopo kijijini iv. Kuongeza tija katika kilimo	i. Kulima ekari 25 za mpunga ii. Kuvuna kilo 134,750 za mpunga	i. Kuongezeka kwa chakula kijijini ii. Kuongezeka kwa mapato ya wanakijiji	i. Halmashauri ya kijiji ii. Idara ya mazingira iii. Idara ya kilimo iv. Idara ya maji	i. Nguvu kazi (wanakijiji) ii. Vibanio vya maji (vya kienyeji watajenga wanakijiji) iii. Vibanio 10 vya kitaalamu (msaada wa halmashauri ya kijiji)
4.	Wafugaji	Uboreshaji ng'ombe wa kienyeji kuwa wa maziwa	i. Kuwepo kwa eneo dogo la malisho	i. Kuinua kipato cha wafugaji ii. Kupunguza idadi ya mifugo ili kukidhi eneo lililopo	i. Kuboresha afya ya jamii (kwa kunywa maziwa) ii. Kuinua kipato cha mfugaji	i. Idara ya kilimo na mifugo ii. Idara ya maji iii. Idara ya ardhi iv. Tassisis za	i. Idara ya kilimo na mifugo ii. Mashirika ya mikopo (madume bora)

				iii. Kuongeza uzalishaji wa maziwa	iii. Kupata mbolea kwa ajili ya kilimo iv. Kupunguza uharibifu wa mazingira (ardhi)	kifedha v. Mashirika ya kidini vi. NGOs	iii. Wafugaji wenyewe (ardhi ya malisho)
5.	Kamati ya hifadhi	Mradi wa kupanda miti	i. Ongezeko la idadi ya watu (baada ya miaka 10) i. Ongezeko la matumizi ya rasilmali miti (kuni, kamba, ujenzi, dawa, samani n.k)	i. Kuotesha miche 1400 ii. Kutoa elimu ya upandaji miti na usimamizi wake kwa wananchi iii. Kutoa elimu ya uvunaji rasilimali miti na matumizi yake	i. Jamii kupata rasilimali miti kwa urahisi ii. Kuzuia mmomonyoko wa udongo iii. Kuboresha hali ya hewa iv. Kuwezesha kufanyika kwa biashara ya kuni na mbao v. Kupunguza umbali wa kutafuta kuni kwa kina mama vi. Kuongeza baianuai katika msitu wa sili	i. Idara ya misitu ii. Idara ya kilimo iii. Maendeleo ya maendeleo ya jamii iv. Shule za msingi v. Taasisi za dini vi. Serikali ya kijiji	i. Ardhi ii. Mbegu za miti iii. Maji iv. Mabomba v. Majembe, chepe vi. Chekeche, makarai, samadi vii. Viriba (majani ya migomba) iii. Fedha, watu
6.	Kundi la vijana	Benki tofari	i. Kupata ajira ya kujiajiri	i. Kubadilisha wanakikundi toka hali mbaya kwenda hali nzuri	i. Kupata fedha za -Kusomesha watoto -Kujikwamua kiuchumi	i. Benki kata (SACOS) ii. Halmashauri ya kijiji	i. Udongo ii. Maji iii. Misitu iv. Pumba/maranda v. Watu
7.	Kundi la kina mama	Mradi wa mama lishe	i. Hali duni ya maisha	i. Kuongeza kipato katika familia	i. Kusomesha watoto ii. Kuongeza lishe katika familia iii. Kupata huduma za afya kiurahisi	i. Idara ya afya ii. Halmashauri ya kijiji	i. Michango ya pesa toka kwa wanakikundi ii. Mkopo toka chama cha kuweka na kukopa cha kata
8.	Utawala	Mradi wa ofisi ya kijiji	i. Mazingira mabaya ya kufanyia kazi na kutunza kumbukumbu kutokana na kijiji kukosa ofisi ii. Kuongezeka kwa gharama za kukodi majengo (kwa ajili ya ofisi)	i. Kuboresha utendaji kazi na utunzaji wa kumbukumbu za kijiji ii. Kupunguza usumbufu wa kuhama hama	i. Kuwa na eneo (jengo) maalum la kufanyia kazi (ofisi) ii. Kutunza vizuri kumbu kumbu mbali mbali za kijiji	i. Halmashauri ya kijiji ii. Halmashauri ya wilaya iii. WDC iv. Baraza la wazee v. Wakuu wa dini	i. Watu ii. Ardhi iii. Maji iv. Misitu v. Fedha

4.4 Majumuisho

Muwezeshaji (Dr Lerise) alifanya majumuisho ya siku ya nne kwa kuwaambia washiriki kuwa katika mafunzo ya leo tumeona mambo mengi muhimu. Aliyataja yafuatayo kuwa ni miongoni mwa mambo hayo:

i. Kupitisha mpango ni kazi ngumu inayohitaji sifa nyingi muhimu (kv uzoefu, umakini, ukweli, uaminifu, n.k.)
ii. Wanaopitisha mpango ni wanakijiji na wala si serikali kuu
iii. Ni vizuri mwenyekiti akaufahamu vizuri mpango ili auendeshe mkutano kwa ufanisi
iv. Viongozi wanatakiwa kujiamini na kutoa ufafanuzi mzuri kwa wananchi (wanakijiji)
v. Ili kurahisisha upitishaji wa mpango ni muhimu kupanga kwa makini na kutumia busara
vi. Katika kupitisha mpango ni muhimu kutumia wajumbe wa halmashauri ya kijiji kufafanua hoja mbalai mbali, na wajumbe hao wanatakiwa kutetea mpango
vii. Katika mkutano mkuu ni muhimu kuheshimu uhuru wa kutoa mawazo kwa kila mjumbe wa mkutano (wanakijiji)
viii. Ili kupata mahudhurio mazuri ni muhimu kutangaza mkutano kwa wanakijiji (tarehe, siku, saa, na sehemu ya kukutania)
ix. Upitishaji wa mpango usiwe wa kulazimisha na mpango usionekane kama tayari ni uamuzi
x. Ni muhimu kuwapo na utaratibu wa kufanya marejesho kwa wananchi ili wajue nini kinaendelea katika masual waliyoyafanyia maamuzi
xi. Baadhi ya wananchi wanakuwa wabinafsi katika mkutano mkuu kwa kulazimisha maslahi yao kupitishwa
xii. Baadhi ya wanakijiji wanajali zaidi posho kuliko hoja yao na maslahi ya kijiji

Akimalizia majumuisho ya siku ya nne ya mafunzo Dr Lerise alibainisha mambo muhimu ya kuzingatia kuhusu maandalizi ya mkutano mkuu wa kijiji kwa waendesha mkutano na washiriki kuwa ni haya yafuatayo:

Waendesha mkutano

i. Kutoa taarifa ya mkutano
ii. Kutoa mwaliko kwa wadau muhimu
iii. Kufanya kikao cha maandalizi
iv. Kupanga tarehe na muda wa mkutano
v. Kuchagua eneo la mkutano
vi. Kuwa na uwezo wa kuendesha mikutano kwa kuzingatia utaratubu wa ushirikishwaji
vii. Kuwa na uwezo wa kuandaa mihutasari inayoonesha michango ya kila mshiriki bila upendeleo
viii. Kuwa na uzoefu wa kuandaa na kuendesha mikutano mikuu

Washiriki/wadau

i. Wamejiandaa vipi kuchangia katika mkutano na siyo kuhudhuria tu
ii. Wameandaliwa vipi kuchangia katika mkutano,
iii. Wamepata taarifa ya mkutano lini,
iv. Wameuona mpango kabla au wanauona kwenye mkutano,

v. Wanauwezo wa kuuchambua huo mpango au wamesaidiwa kuuelewa
vi. Wameondolewa hofu ya kuuliza
vii. Wana uzoefu wa kuhudhuria na kuchangia katika mikutano mikuu

Kuwasilisha na kupitisha mpango – Mkutano mkuu wa kijiji

SIKU YA TANO **IJUMAA 9/11/2007**

5.1 Mchakato wa kuanzisha mradi wa hifadhi ya jamii (WMA)

Lengo

Kufahamu utaratibu na hatua za kufuata katika uanzishaji wa mradi wa hifadhi ya jamii

Utangulizi

Washiriki wote walikaa katika chumba cha mafunzo na muwezeshaji (Dr Kideghesho) akawasilisha mada kuhusu mchakato wa kuanzisha mradi wa hifadhi ya jamii (WMA). Washiriki walipata nafasi ya kuuliza maswali na kuomba ufafanuzi pale ambapo walikuwa hawajaelewa.

Mbinu za kujifunza

i. Mawasilisho ya mada
ii. Maswali na majibu
iii. Ufafanuzi wa mada

Mawasilisho na majadiliano

Katika kuwasilisha mada muwezeshaji (Dr Kideghesho) alitaja hatua muhimu za kufuatwa ili kuanzisha eneo la hifadhi ya jamii (WMA) ambalo litatambulika kisheria. Alizitaja hatua hizo kuwa ni:

i. Wanakijiji kuhamasishwa kuhusu umuhimu, gharama, faida, haki na dhima yao katika kulinda maliasili, na taratibu za uteuzi wa maeneo ya jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori
ii. Halmashauri ya kijiji kupendekeza katika kikao cha baraza la wanakijiji eneo linalofaa kutengwa kwa ajili ya jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori
iii. Wanakijiji wanaotarajia kuanzisha eneo lajumuiya ya hifadhi ya wanyamapori kuunda chama wakilishi cha jumuiya
iv. Chama wakilishi cha jumuiya kuwakilisha maombi kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori
v. Mkurugenzi kukusanya taarifa kuhusu chama wakilishi kilichopendekezwa na kuidhinisha au kukataa eneo lililopendekezwa
vi. Mkurugenzi kuwasilisha ombi pamoja na mapendekezo yake kwa Waziri wa Maliasili na Utalii
vii. Waziri wa maliasili na utalii kutangaza eneo la jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori na kusababisha kuchapishawa kwa chama wakilishi na eneo lililoteuliwa katika gazeti la serekali

Baada ya hatua hizi kufuatwa na kukamilika eneo husika litakuwa ni eneo la jumuiya la hifadhi ya wanayamapori linalotambuliwa kisheria.

Rejea

Hand out Namba 7 – Jamii na uhifadhi (Community Conservation)

5.2 Changamoto katika kuandaa, kupitisha na kutekeleza sheria ndogo

Lengo

Kufahamu umuhimu wa sheria ndogo katika utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi wa kijiji

Utangulizi

Washiriki waligawanywa katika makundi makubwa mawili:

(a) Washiriki katika ngazi ya kijiji
(b) Washiriki katika ngazi ya kata na wilaya

Kila kundi lilitengeneza makundi matatu yaliyotakiwa kujadili na kuwasilisha changamoto katika *kuandaa, kupitisha na kutekeleza* sheria ndogo katika ngazi husika. Kwa ujumla kulikuwa na makundi sita (6) yaliyojadili na kuwasilisha mada ya changamoto za sheria ndogo. Washiriki ngazi ya vijiji makundi 3 yaliyoangalia changamoto katika kuandaa, kupitisha na kutekeleza sheria ndogo, na washiriki ngazi ya wilaya na kata makundi matatu yaliyoangalia pia changamaoto za kuandaa, kupitisha na kutekeleza sheria ndogo katika ngazi ya kata na wilaya.

Mbinu za kujifunza

i. Vikundi kazi
ii. Majadilano katika vikundi
iii. Mawasilisho, maswali na majibu
iv. Majadiliano ya washiriki kwa ujumla

Mawasilisho na majadiliano

Washiriki katika makundi waliwasilisha majadiliano yao kwa washiriki wote na wakaulizwa na kujibu maswali mbali mbali. Kwa ujumla ilionekana kuwa kila eneo katika maeneo matatu ya kuandaa, kupitisha na kutekeleza sheria ndogo lina ugumu wake. Washiriki wakatakiwa kuwa makini na masuala ya sheria. Suala hilo linaelezwa kwa kina katika kipengele kinachofuata (kutunga sheria ndogo). Jedwali Namba 5.1 linaelezea matokeo ya mawasilisho kuhusu sheria ndogo.

Jedwali Namba 5.1: Changamoto katika kuandaa, kupitisha na kutekeleza sheria ndogo

Kundi	Changamoto za sheria ndogo		
	Kuandaa	**Kupitisha**	**Kutekeleza**
Ngazi ya kijiji	i. Mpangilio wa sheria ndogo unaingiliana na sheria mama ii. Waandaaji kutaka mawazo yao ndiyo yawe sheria badala ya maoni ya mkutano mkuu iii. Kutozingatiwa kwa akidi ya wananchi iv. Waandaaji kuandaa sheria inayowafurahisha badala ya itakayowanufaisha	i. Wajumbe hugoma kupitisha sheria iliyowafurahisha waandaaji na kutoangalia manufaa kwa wananchi ii. Kutozingatiwa kwa akidi ya wananchi	i. Uelewa mdogo wa sheria ii. Migongano/tofauti za kisiasa miongoni mwa wajumbe iii. Mila na desturi za mahali inabidi ziangaliwe iv. Kuna usimamizi mdogo wa sheria v. Mawasiliano duni (vyombo vya usafiri) yanakwamisha utekelezaji
Ngazi ya kata na wilaya	i. Kukosekana kwa mwanasheria/wanasheria katika Halmashauri ya wilaya ii. Kutofahamu sheria mama zinazosimamia sheria ndogo	i. Tofauti za kisiasa miongoni mwa wajumbe ii. Mila na desturi za wenyeji iii. Wajumbe kutofahamu sheria mama iv. Wajumbe kutokuwa naelimu ya msingi ya sheria v. Mahudhurio duni katika vikao vya kupitisha sheria vi. Kukosekana kwa wanasheria katika vikao vya upitishaji sheria vii. Ukosefu wa fedha za kufanya vikao katika wakati muafaka	i. Ukosefu wa wanasheria ili kutoa ufafanuzi wa kisheria ii. Uelewa mdogo wa sheria kwa wananchi iii. Kulindana na kuoneana haya kwa wasimamizi wa sheria iv. Kuwapo kwa tabia ya kutokujali madhara ya kutofuata sheria v. Wajumbe wa baraza la kata kutoelewa majukumu yao vizuri vi. Upungufu wa vitendea kazi

5.3 Kutunga sheria ndogo (Resource persons)

Lengo

Kufahamu mipaka na majukumu ya watendaji kuhusu utungaji na utekelezaji wa sheria ndogo

Utangulizi

Katika mada hii washiriki wawili ambao ni wataalamu katika masuala ya kisheria (resource persons) waliandaa na kuwasilisha mada kwa washiriki wengine. Baada ya mawasilisho washiriki waliuliza maswali na kuomba ufafanuzi wa vifungu mbali mbali vya kisheria vinavyohusiana na utendaji wao wa kazi za kila siku kama wasimamizi wa mipango na watekelezaji wa maamuzi ya wananchi.

Mbinu za kujifunza

i. Mawasilisho ya mada
ii. Maswali na majibu
iii. Majadiliano ya washiriki kwa ujumla

Mawasilisho na majadiliano

Wawasilishaji mada (Mr Manyonyi na Mr Yamungu) waliwasilisha mada hii kwa kufuata vipengele mbali mbali muhimu kama vinavyooneshwa hapo chini.

Mamlaka ya Halmashauri ya kijiji kutengeneza sheria ndogo

Muwasilishaji (Mr Manyonyi) aliwabainishia washiriki kuwa Halmashauri ya kijiji imepewa mamlaka ya kutunga sheria ndogo kwa ajili ya kusaidia na kutekeleza majukumu au kazi zake. Mamlaka haya yanatolewa na kifungu Na. 163 cha sheria ya Serikali za Mitaa Namba 7 ya mwaka 1982.

Hatua za kuandaa sheria ndogo

Mr Manyonyi aliendelea kuwafahamisha washiriki kuwa kifungu Na 164 cha Sheria Na 7 ya mwaka 1982 kinatoa utaratibu unaotakiwa kufuatwa na Halmashauri ya kijiji katika kutunga sheria ndogo. Utaratibu huo ni huu ufuatao:

1. Kuitisha mkutano mkuu wa kijiji na kutoa mapendekezo ya kutunga sheria ndogo husika
2. Mkutano mkuu kuchambua na kupitisha mapendekezo kama yalivyotolewa na Halmashauri au kuyafanyia marekebisho kabla ya kuyapitisha ili yawe sheria ndogo (By law)
3. Ushauri wa wananchi au maoni yaliyotolewa katika mkutano mkuu ni lazima yazingatiwe
4. Sheria ndogo iliyopitishwa pamoja na muhtasari wa mkutano mkuu viwasilishwe Halmashauri ya wilaya ambayo ina mamlaka juu ya kijiji husika
5. Kwa kuzingatia ushauri wa Halmashauri ya kijiji, Halmashauri ya wilaya itapitisha sheria hiyo ndogo na itaanza kutumika rasmi siku ilipotangazwa na Halmashauri ya wilaya (kif 164 (2) Sheria Na 7 ya 1982)

Akiendelea na mawasilisho Mr Manyonyi alisema kuwa sheria ndogo haziruhusiwi kuathiri au kukinzana na sheria ya Serikali za mitaa Na 7 ya 1982, au sheria nyingine yoyote iliyotungwa katika nchi hii. (kif 164(3) Sheria Na 7 ya 1982).

Ushahidi wa kuthibitisha kukubalika kwa sheria ndogo(By Law) kwaHalmashauri ya kijiji

Muwasilishaji (Mr Manyonyi) aliwafahamisha washiriki kuwa uhalali wa sheria ndogo unathibitishwa na Halmashauri ya kijiji. Uthibitisho au ushahidi huo unapatikana kwa kuwepo muhuri wa Halmashauri ya kijiji katika sheria ndogo au sheria ndogo kusainiwa na katibu wa Halmashauri ya kijiji au mtu mwingine mwenye mamlaka katika Halmashauri hiyo (kif Na 166 Sheria Na 7 ya 1982). Tofauti na hivyo sheria hiyo ndogo itakuwa haina uthibitisho kama ni sheria halali.

Utekelezaji wa sheria ndogo katika kijiji

Akiendelea na uwasilishaji wa mada muwasilishaji (Mr Yamungu) aliwafahamisha washiriki kuwa utekelezaji wa sheria ndogo katika kijiji unafanywa na kamati tatu zifuatazo:

1. Kamati ya mipango na fedha
2. Kamati ya huduma za jamii na shughuli za kujitegemea
3. Kamati ya ulinzi na usalama

Kamati hizi zina jukumu la kutekeleza na kulinda sheria ndogo kwa kudhibiti matendo kama wizi, uharibifu wa mazingira, shughuli haramu za uzalishaji kama uvuvi haramu, uchimbaji madini usioruhusiwa n.k)

Adhabu zitolewazo kwa kuvunja sheria ndogo

Akimalizia mawasilisho ya mada muwasilishaji (Mr Yamungu) aliwafahamisha washiriki kuwa sheria ndogo nazo zina ukomo wa mamlaka. Kwa mujibu wa kifungu cha 167 cha sheria Na 7 ya 1982, mtuhumiwa aliyevunja sheria ndogo anatakiwa kulipa faini isiyozidi shilngi elfu hamsini (50,000/=). Hii ina maanisha kuwa sheria ndogo haina mamlaka ya kutoa kifungo cha aina yoyote kwa mtuhumiwa.

Akimalizia alisema kuwa mtuhumiwa anahaki ya kukata rufaa kupinga adhabu aliyopewa kwa kutumia sheria ndogo. Kama ikithibitika kuwa hakutenda kosa atastahiki kulipwa fidia ambayo italipwa na Halmashauri ya kijiji chenye mamlaka ya kutunga sheria, au chombo kilichotumika kumtoza faini mtuhumiwa, au kamati yoyote iliyohusika kusikiliza mashauri ya mtuhumiwa huyo.

Ufafanuzi huu wa kisheria ulileta mjadala mkubwa kutoka kwa washiriki. Washiriki wengi ambao ni watendaji vijijini walisema kuwa kama hivyo ndivyo sheria inavyosema basi wao hawana kazi au kazi yao itakuwa ngumu sana. Walisema kuwa wananchi vijijini wanatumia mwanya wa sheria ili kufanya makosa kama vile uharibifu wa maliasili, vianzo vya maji na uchimbaji wa madini wakitegemea kuwa hawawezi kufungwa bali watalipa faini tu.

Wakielezea zaidi kutoridhishwa kwao na ufafanuzi huu wa kisheria washiriki hao walisema kuwa sheria mama nazo zinachangia kuwafanya wananchi vijijini waendelee kufanya makosa kwa kuwa wanajua sheria hizo zinatoa faini ndogo sana wakati mwingine hata shilingi elfu mbili (2,000/=). Walisema hali hii inawakatisha tamaa kwa kuwa wahalifu wakishaachiwa na mahakama hurudi kwao na kujisifu kuwa hawawawezi, jambo ambalo linawafanya pengine wasite kuwakamata wanaporudia makosa yale yale.

Wakijibu hoja za washiriki watoa mada walisema kuwa hivyo ndivyo sheria inavyosema na wala si maneno yao. Wakaongezea kuwa kwa sasa hakuna la kufanya ila kufuata sheria inavyosema.

Jambo la muhimu kwa watendaji vijijini ni kuendelea kuwalalamikia watunga sheria wetu ili wabadilishe sheria na vifungu vya sheria vilivyopitwa na wakati.

Mawasilisho ya sheria ndogo - mshiriki mtaalamu wa sheria (resource person)

5.4 Mpango wa utekelezaji (Action plan)

Lengo

Kuhusianisha mafunzo na matendo katika utendaji kazi wa washiriki

Utangulizi

Kabla ya kumaliza mafunzo washiriki walitakiwa kueleza nini watakachokwenda kufanya katika maeneo yao ya kazi baada ya kupata mafunzo. Kwa maneno mengine walitakiwa kueleza kile walichojifunza watakitumiaje katika utendaji wao wa kazi za kila siku. Walitakiwa kuandika kurasa mbili za mpango wa utekelezaji na kuziwasilisha siku iliyofuata (siku ya mwisho ya mafunzo). Katika kufanya zoezi hilo washiriki walitakiwa kujibu swali lifuatalo:

1. Baada ya mafunzo haya ni mambo gani unatarajia kwenda kuyafanya? (Zingatia uwezo wako wa kutekeleza)
   (a) Wewe mwenyewe katika sehemu yako ya kazi
   (b) Ninyi kama taasisi (yaani kijiji, kata, tarafa na wilaya)

Mbinu za kujifunza

i. Kuandika mipango
ii. Mawasilisho ya mipango iliyoandikwa

Mawasilisho

Washiriki waliwasilisha mipango iliyoandikwa siku inayofuata. Mipango ilikusanya na kutunzwa pamoja kwa ajili ya kutathminiwa na kuwianishwa ili kupata mipango binafsi na mipango ya ujumla kwa taasisi. Mawasilisho ya mipango hiyo yanaoneshwa katika Jedwali Namba 5.2 hapo chini.

5.5 Majumuisho

Katika kujumuisha mada hii muwezeshaji (Dr Kideghesho) aliwafahamisha washiriki kuwa ni muhimu kufuata hatua zote zilizobainishwa hapo juu wakati wa kutenga maeneo ya ushoroba (WMA) katika vijiji vyao. Kwa kufanya hivyo wataepusha migongano isiyo ya lazima kati ya viongozi na wanavijiji.

Ilionekana pia sheria mama zinanyima nguvu na mamlaka kwa sheria ndogo zinazotungwa katika ngazi za vijiji na wilaya. Ilishauriwa kuwa mapendekezo ya kuwezesha uboreshaji wa utungaji wa sheria ndogo (ili ziwe na nguvu, ziogopwe na ziheshimiwe) yafanywe na washiriki katika maeneo yao ya kazi kwa kutumia vikao husika. Kwa mfano ilipendekezwa kuwa badala ya kusema faini inayotolewa na sheria ndogo isizidi shilingi elfu hamsini (50,000/=), sheria iseme kuwa faini iwe si chini ya elfu hamsini.

Jedwali Namba 5.2: Mpango wa utekelezaji (Action plan)

Mipango binafsi		Mipango ya jumla	
Watendaji vijijini	**Wataalamu kata na wilaya**	**Vijiji**	**Kata na wilaya**
i. Kushauriana na wenyeviti wengine wa vijiji kuhusu kutambua mipaka ya vijiji ii. Kuhamasisha jamii kuunda jumuiya kupitia mradi wa ushoroba iii. Kuhamasisha kuibua miradi mbali mbali (kutoka mpango wa matumizi ya ardhi) kwa pamoja iv. Kuibua miradi binafsi inayoendana na mipango ya vijiji mf. Mradi wa upandaji miti	i. Wataalamu kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa uhifadhi ii. Kusaidia katika kutenga maeneo ya uhifadhi iii. Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu na aina nzuri ya ushirikishwaji iv. Kuelimisha wananchi juu ya mipaka ya sheria ndogo na kusisitiza kuwa kutojua sheria si utetezi v. Kuhamasisha viongozi wa vijiji kubandika sheria ndogo kwenye mbao za matangazo na sehemu za mikusanyiko ili wanakijiji wazielewe vi. Kushawishi na kuhamasisha jamii kukubali na kupitisha mpango wa matumizi ya ardhi vii. Kuandaa ripoti ya mafunzo na kuwasilisha kwenye kikao cha wakuu wa idara viii. Kusimamia sheria ndogo kwa umakini zaidi kuliko hapo mwanzo ix. Kutoa ushauri kwa mkurugenzi wa Halmashauri atafute uwezekano wa kutoa mafunzo kama haya kwa vijiji vilvyo nje ya mradi wa ushoroba x. Kumshauri mkurugenzi afanye utaratibu wa kupima kijiji kimoja au viwili kwa mwaka kutegemeana na bajeti	i. Kuitisha mikutano ya hadhara kuwataarifu wananchi kuhusu tuliyojifunza na umuhimu wake ii. Kuitisha vikao vya ngazi mbali mbali (kamati za kijiji, wazee maarufu, vijana n.k) kuwataarifu kuhusu mafunzo ili kuboresha ushirikishwaji iii. Kuanzisha taratibu za uandaaji wa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji iv. Kushirikisha jamii katika utungaji wa sheria ndogo za matumizi bora ya ardhi ya kijiji v. Kuhakikisha mipango itakayopangwa inazingatia sheria ili itekelezeke	i. Kuhakiki rasilimali zilizopo ndani ya maliasili ya wilaya ii. Kushirikiana na wataalamu wengine wa kata kuandaa mipango ya matumizi bora ya maliasili iii. Kuitisha vikao vya WDC na kuelezea yote yaliyofundishwa iv. Kupanga ratiba ya kutembelea vijiji na kuitisha mikutano mikuu ili kuwataarufa wananchi kuhusu mafunzo v. Kushirikisha vijiji, tarafa na wilaya katika kufuatilia uandaaji wa mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi vi. Kukutana na watendaji ngazi ya kata na vijiji ili kuandaa taratibu za uandaaji wa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji vii. Kuviwezesha vijiji kupimwa na kupata vyeti vya ardhi ya kijiji viii. Kuchambua sera mbali mbali na kuwianisha ili kuona kama zinakinzana ix. Wataalamu wa sekta mbali mbali kujadili sera zote kwa pamoja na kuangalia vigezo vinavyofanana ili na kuvipa vijiji ili vitumie katika kuandaa mipango yao ya matumizi ya ardhi

6.1 Mpango wa mfano (Ripoti)

Lengo

Kupata ufahamu juu ya vitu vya lazima kuwepo katika repoti ya mpango wa matumizi bora ya ardhi ambavyo hutoa taarifa na ufafanuzi juu ya mpango na kuuwezesha kupitishwa na mamlaka husika

Utangulizi

Ili kuwawezesha washiriki kuelewa vizuri mpango wa matumizi bora ya ardhi, mpango halisi uliopitishwa na mamlaka husika uliwasilishwa kwa washiriki. Mpango wa kijiji cha Makundusi kilichopo wilaya ya Serengeti, mkoa wa Mara ulichaguliwa kuwa mpango wa mfano na kuoneshwa kwa washiriki. Mpango huu ulipatikana wizara ya Ardhi Dar es Salaam ambako mipango hupelekwa na kupitishwa baada ya kupitia ngazi za chini za upitishaji mpango.

Mbinu za kujifunza

i. Mawasilisho toka kwa mtoa mada
ii. Maswali na majibu
iii. Ufafanuzi toka kwa wakufunzi

Mawasilisho na majadiliano

Katika mawasilisho muwezeshaji (Mr Ka'Bange) alielezea vitu muhimu vilivyomo katika mpango wa kijiji cha Makundusi, kasoro za mpango, na mfano mzuri wa matumizi ya vifungu vya sheria katika mpango. Muwezeshaji alisema kuwa mpango wa matumizi ya ardhi wa Kijiji cha Makundusi unaonesha vipengele muhimu vifuatavyo:

i. Utangulizi-(unaoonesha jina la kijiji, kata, tarafa, wilaya n.k.)
ii. Mipaka ya kijiji –(inayooneshwa kwa kutumia mawe ya kijiji)
iii. Maumbile ya kijiografia (sura ya nchi, mbuga na mabonde, miinuko, milima, aina za udongo, uoto wa asili)
iv. Matumizi ya ardhi iliyopo (makazi, kilimo, malisho, vyanzo vya maji, eneo la nishati ya kuni, uwindaji)
v. Takwimu za kiuchumi jamii (idadi ya watu)
vi. Tathmini ya uwezo wa ardhi kwa matumizi mbali mbali
vii. Chaguzi za kuboresha uzalishaji wa ardhi (kuchagua VLUM na PLUM)
viii. Mapendekezo ya mpango wa matumizi bora ya ardhi-Rasimu ya matumizi bora ya ardhi ya kijiji (iapendekeza kuwepo maeneo ya makazi, kilimo, malisho, misitu ya kuni, vyanzo vya maji, eneo la matambiko, hifadhi ya wanyamapori na machimbo)
ix. Mikakati ya utekelezaji
x. Viambatanisho (Sheria ndogo, mihutasari ya vikao)

Mifano halisi

Mpango wa kijiji cha makundusi umeonesha baadhi ya mambo yaliyofundishwa na kujadiliwa katika mafunzo. Baadhi ya mambo hayo ni:

i. Matumizi ya kifungu Na 11 cha Sheria ya Ardhi ya 1999 – kijiji kitafanya makubaliano na vijiji jirani juu ya matumizi ya ardhi na rasilimali za pamoja (uk 9)
ii. Ardhi ya kijiji ni ndogo kuliko mahitaji. Mahitaji ya ardhi ni hekta ***54,476*** ukubwa wa kijiji ni hekta ***21,103***, hivyo kuna upungufu wa hekta ***33,373***

Kasoro za mpango

Mpango wa kijiji cha Makundusi una kasoro mbali mbali ambazo baadhi ya kasoro hizo ni:

i. Kutotaja idadi ya watu na kaya katika kijiji (ambazo ni takwimu za msingi katika kuandaa mpabgo)
ii. Kutaja mipaka kwa kutumia mawe ya kijiji (beacons) na siyo majirani katika pande zote.
iii. Kutofuata mpangilio wa vipengele muhimu vya mpango
iv. Sheria ndogo zinatoa kifungo na faini ya zaidi ya shiling elfu hamsini (mpaka laki tatu)

Vitu vya muhimu kuwapo katika mpango wa matumizi bora ya ardhi

Akimalizia mawasilisho ya mada hii muwezeshaji (Mr Ka'Bange) alibainisha vitu muhimu vinavyotakiwa kuwapo katika mpango wa matumizi ya ardhi. Alivitaja vitu hivyo kuwa ni hivi vifuatavyo:

I. Utangulizi (unaoonesha vitu vifuatavyo)
-Jina la kijiji, kata, tarafa, wilaya na mkoa
-Maelezo mafupi kuhusu mpango mf. ulianza lini, msukumo ulitoka wapi n.k.
-Mpango ulivyotayarishwa (utaratibu shirikishi, kutumia watendaji wa wilaya, washauri n.k

II. Mipaka ya kijiji
-Majirani pande zote: kaskazini, kusini, mashariki na magharibi
-Eneo la kijiji kwa ujumla katika hekta au kilomita za mraba

III. Hali halisi ya kijiji
-Maumbile ya kijiografia (milima, mabonde, uoto, aina za udongo, mito, maziwa n.k)
-Matumizi ya sasa ya ardhi (makazi, miundo mbinu, kilimo, malisho, n.k.)

IV. Takwimu za uchumi jamii
-Idadi ya watu (wanaume, wanawake, watoto, walemavu)
-Idadi ya kaya katika kijiji
-Shughuli za uchumi kijijini na idadi ya wahusika

V. Tathmini ya uwezo wa ardhi kwa matumizi mbali mbali
-Utaratibu wa kitaalamu wa kutathmini mahitaji ya ardhi
-Kutathmini na kutenga maeneo

VI. Mapendekezo ya mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji
-Kutenga maeneo mbali mbali km kilimo, makazi, malisho, serikali ya kijiji, ushoroba n.k

VII. Rejea
-Orodha ya vitabu, majarida na nyaraka nyingine zilizotumiwa katika kuandaa mpango

VIII. Viambatanisho
-Taratibu za uchaguzi wa VLUM na PLUM, Sheria ndogo, mihutasari ya vikao n.k.

6.2 Mpango wa mfano (Ramani)

Lengo

Kupata ufahamu juu ya vitu vya lazima kuwepo katika ramani ya mpango wa matumizi bora ya ardhi ambao husaidia kuuwezesha mpango kupitishwa

Utangulizi

Ramani ya kijiji cha Ngereiyani kilichopo wilaya ya Monduli mkoa wa Arusha ilichaguliwa kuwa ramani ya mfano na kuwasilishwa kwa washiriki. Ramani hii ilipitishwa na wizara ya ardhi kuwa ni sehemu ya mpango wa kijiji hicho.

Mbinu za kujifunza

i. Mawasilisho toka kwa mtoa mada
ii. Maswali na majibu
iii. Ufafanuzi toka kwa wakufunzi

Mawasilisho na majadiliano

Muwezeshaji (Mr Ka'Bange) aliwasilisha ramani ya kijiji cha Ngereiyani kwa kueleza mambo yanayooneshwa na ramani hiyo, mapungufu yake na mambo muhimu yanayotakiwa kuwapo katika ramani nzuri ya mpango. Pia alielezea matumizi ya rangi za mipango miji katika kuandaa ramani ya mpango.

Aliainisha mambo muhimu yaliyooneshwa katika ramani ya kijiji cha makundusi kuwa ni haya yafuatayo:

i. Makazi/Kilimo/Malisho
ii. Malisho wakati wa kiangazi
iii. Malisho wakati wakati wote
iv. Makazi na kilimo
v. Misitu/Wanyamapori/Malisho

Upungufu katika ramani ya Ngereiyani

Muwezeshaji (Mr Ka'Bange) alitaja mapungufu yafuatayo katika ramani ya kijiji cha Ngereiyani:

i. Kuchanganya matumizi yanayokinzana (Kilimo na malisho)
ii. Kutokuwa na uwiano wa maeneo (eneo lilotengwa kwa malisho wakati wa kiangazi limekuwa kubwa sana (takriban nusu ya eneo lote la kijiji) ukilinganisha na maeneo mengine kama kilimo)

Vitu muhimu kuwapo katika ramani ya mpango

Akimalizia mawasilisho ya ramani ya Ngereiyani Mr Ka'Bange aliainisha vitu muhimu vinavyotakiwa kuwapo katika ramani nzuri ya mpango kuwa ni hivi vifuatavyo:

i. Iwe na ufunguo – unaoonesha vitu vilivyomo katika ramani
ii. Ioneshe uelekeo – Kaskazini na Kusini
iii. Iwe na kipimio – cha kupimia umbali na eneo katika ramani
iv. Iwe na uwiano katika maeneo yaliyotengwa
v. Itofautishe maeneo yanayokinzana (km Kilimo na mifugo, maeneo ya Burudani na Ibada)

vi Itumie rangi za mipango miji

-Makazi	*Njano*
-Uoto	*Kijani nzito*
-Taasisi (mf Shule)	*Nyekundu*
-Biashara	*Bluu nzito*
-Mito, bahari, maziwa	*Bluu nyepesi*
-Viwanda	*Zambarau*
-Barabara	
Lami	*Nyeusi*
Changarawe/udongo	*Rangi ya udongo*

Vii Ioneshe imetayarishwa na nani (Halmashauri ya wilaya, uongozi wa kijiji, wizara nk)

6.3 Tathmini ya mafunzo

Lengo

Kutoa fursa kwa washiriki kutoa maoni juu ya umuhimu wa mafunzo waliyopata katika kuboresha utendaji wao wa kazi na maisha kwa ujumla, ubora wa wawezeshaji na mbinu zilizotumika, upungufu uliojitokeza, na mambo ya kuboreshwa katika mafunzo kama haya.

Utangulizi

Washiriki walipewa fomu yenye maswali saba yanayohusu mambo mbali mbali yaliyofanyika katika mafunzo na walitakiwa kujaza na kuwasilisha hapo hapo. Jumla ya fomu 73 zilijazwa na kukusanywa. Mchanganuo wa maoni hayo ya washiriki unaoneshwa katika Kiambatanisho Namba 4 kinachoonesha Tathmini ya mafunzo.

Mawasilisho

Washiriki waliwasilisha/walikusanya fomu walizogawiwa baada ya kuzijaza kwa ukamilifu na kujibu maswali yote yaliyokuwamo kwenye fomu hizo.

6.4 Kufunga mafunzo

Baada ya washiriki kufanya tathmini ya mafunzo Meneja mradi wa Ushoroba (Mr Ngomelo) na mwakilishai wa GTZ (Mr Rudi) walitoa hotuba fupi za kufunga mafunzo. Mr Rudi aliwafahamisha washiriki kuwa amefurahi kuona kuwa wamemaliza mafunzo haya kwa mafanikio na akawaomba kutumia ujuzi walioupata katika zoezi linalokuja la kuandaa eneo la ushoroba katika vijiji vyao. Alisema pia wao kwa upande wao wanaendelea na shughuli mbali mbali za ushoroba ambapo kwa sasa wamekwishaandaa CD yenye nyimbo za asili za makabila yaliyopo katika eneo la mto Ruvuma. Akasema kuwa CD hiyo itasaidia kulitangaza zaidi eneo la ushoroba duniani kote.

Kwa upande wake Meneja mradi wa Ushoroba alisema kuwa alikuwa anawaangalia washiriki wakati wakiendelea na mafunzo na kuona jinsi walivyojifunza kwa bidii na anatarajia kuwa wamejifunza mambo mengi sana yatakayosaidia katika shughuli ya utengaji wa maeneo ya ushoroba katika vijiji vyao. Aliwaomba pia wakawe walimu wa kuwafundisha wale ambao hawakupata nafasi ya kushiriki katika mafunzo haya mambo yote muhimu waliyojifunza. Aliwatakia washiriki safari njema ya kurudi katika vijiji vyao na kutamka kuwa mafunzo YAMEFUNGWA RASMI saa 7:00 kamili mchana.

Kufunga mafunzo

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Namba 1: Ratiba ya mafunzo

SIKU YA KWANZA

Muda	Matukio	Wahusika
2.00 - 2.30	1.1 Washiriki kujiandikisha	Washiriki
2.30 – 3.00	1.2 Sala ya ufunguzi & utambulisho	Dr Lerise Wote
3.00 – 3.45	1.3 Hotuba ya ufunguzi & Majadiliano	Mkuu wa mradi - Ushoroba
3.45 – 4.00	1.4 Mradi wa Ushoroba katika SADC na INWENT	Dr Lerise
4.30 – 5.30	Chai	Wote
5.30. – 5.50	1.4 Video ya mto Ruvuma	Rudi & Madata
5.50 – 6.50	1.5 Matarajio ya washiriki: Vikundi kazi	Washiriki
7.30 – 8.30	Chakula cha mchana	Wote
8.30 – 9.00	1.6 Matarajio ya washiriki: mawasilisho	Washiriki
9.00 – 9.15	1.7 Malengo na mbinu za mafunzo	Dr Kideghesho
9.15 – 9.35	1.8 Sera mbalimbali na dhana ya ushirikishwaji	Dr Lerise
9.35 – 10.30	1.9 Kazi katika vikundi	Washiriki
10.30 – 11.00	1.10 Mawasilisho	Washiriki
11.00 -11.05	1.11 Majumuisho	Dr Lerise
	KUFUNGA MAFUNZO SIKU YA KWANZA	

SIKU YA PILI

Muda	Matukio	Wahusika
2:00 – 2:30	Kujikumbusha mada ya siku ya kwanza	
2:30 – 4:00	Mahusiano/uwiano (horizontal integration) ya mipango mbalimbali katika ngazi ya kijiji (Ukurasa 22, 26) Uwiano ngazi (vertical integration) ya mipango mbalimbali katika ngazi ya kijiji, kata na wilaya	Kazi vikundi
4:00 – 4:30	Chai	
4:30 – 5:00	Muundo wa kisheria na kitaasisi (Legal and Institutional framework)-(PLUP, IWRM WMA)	Mawasilisho, maswali & majibu
5:00 – 7:00	Hatua za Kuandaa mpango shirikishi (PLUP) (Ukurasa 37-45)	Kazi vikundi
7:00 – 8:00	Chakula cha mchana	
8:00 – 8:30	Hatua za Kupitisha na Kutekeleza mpango shirikishi (PLUP) (Ukurasa 45-51)	Mawasilisho, maswali & majibu
8:30 – 9:00	Chai	Wote
9:00 – 11:00	Wajibu na Majukumu ya watendaji katika Mipango Shirikishi na Usimamizi (Roles and responsibilities of actors in PLUP&M) (Ukurasa 52-56)	Kazi vikundi
	KUFUNGA MAFUNZO SIKU YA PILI	

SIKU YA TATU

Muda	Matukio	Wahusika
2:00 – 2:30	3.1 Kujikumbusha tuliyojifunza siku ya pili	
2.30 - 3:00	3.2 Utangulizi wa uhakiki wa Rasilimali	Kidegesho
3.00 - 3:30	3.3 Kuunda makundi 10 ya watu 8 na kujiandaa	Kabange
3.30 - 4:00	Chai	Wote
4.00 - 5:30	3.4 Mafunzo kwa vitendo katika maeneo ya uandaaji mpango	Washiriki Usafiri: Madata
5.30 - 6:30	3.5 Maandalizi kwa ajili ya kuwasilisha	Washiriki
6.30 - 7:30	Chakula cha mchana	Wote
7.30 - 8:45	3.6 Mawasilisho	
8:45 - 10:00	3.7 Kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali	Washiriki vikundi
10:00-10:30	3.8 Mawasilisho	Washiriki vikundi
10:30-11:00	3.9 Majumuisho	Lerise Kidegesho
	KUFUNGA MAFUNZO SIKU YA TATU	

SIKU YA NNE

Muda	Matukio	Wahusika
2:00 – 2:30	4.1 Kujikumbusha tuliyojifunza siku ya tatu	Kideghesho
2.30 - 3:30	4.2 Kutenga maeneo inaendelea	Kazi katika vikundi
3.30 - 4:00	4.3 Kuwasilisha	Washiriki
4.00 - 4:30	Chai	Wote
4.30 - 5:15	4.4 Mambo muhimu ya kuzingatia katika kutenga maeneo	Kideghesho
5.15 - 6:00	4.5 Kuwasilisha mpango kwenye mkutano mkuu ----Maandalizi	Washiriki
6.00 - 7:00	4.6 Kuwasilisha mpango kwenye mkutano mkuu ----Mkutano wenyewe	Washiriki
7.00 - 7:30	4.7 Kuwasilisha mpango kwenye mkutano mkuu ----Majumuisho	Lerise
7.30 - 8:30	Chakula cha mchana	Wote
8.30 - 9:00	4.8 Mambo muhimu ya kuwezesha utekelezaji wa mpango ---Utangulizi	Kideghesho
9:00 - 10:00	4.9 Kuibua miradi kutoka kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi ---Kazi katika vikundi	Washiriki
10:00-10:30	4.10 Mambo muhimu ya kuwezesha utekelezaji wa mpango ---Mawasilisho	Washiriki
10:30-11:00	4.11 Mambo muhimu ya kuwezesha utekelezaji wa mpango ---Majumuisho	Lerise Kideghesho
	KUFUNGA MAFUNZO SIKU YA NNE	

SIKU YA TANO

Muda	Matukio	Wahusika
2:00 – 2:30	5.1 Kujikumbusha tuliyojifunza siku ya nne	Kideghesho
2.30 - 3:00	5.2 Kuibua miradi kutoka kwenye mpango	Kazi katika vikundi
3.00 - 4:00	5.3 Kuwasilisha	Washiriki
4.00 - 4:30	Chai	
4.30 - 6:00	5.4 Mchakato wa kuanzisha mradi wa hifadhi ya jamii (WMA)	Wote
6:00 - 6:30	5.5 Changamoto katika sheria ndogo ndogo za kutekeleza mpango ---Kazi katika vikundi	
6:30 - 7:30	Chakula cha mchana	
7:30 - 8:30	5.6 Changamoto katika sheria ndogo ndogo za kutekeleza mpango ---Kazi katika vikundi	
8:30 - 9:30	5.7 Kutunga sheria ndogo ndogo za kutekeleza mpango ---Majumuisho (Maswali & Majibu)	Resource persons
9:30 – 11:00	7.8 Mpango wa utekelezaji kutokana na mafunzo .....vijiji .....kata .....tarafa .....wilaya ya Namtumbo .....wilaya ya Tunduru	Wote
	KUFUNGA MAFUNZO SIKU YA TANO	

SIKU YA SITA

Muda	Matukio	Wahusika
2:00 – 2:30	6.1 Kujikumbusha tuliyojifunza siku ya tano	Kideghesho
2.30 - 3:00	6.2 Kuwasilisha mipango ya utekelezaji baada ya mafunzo	Washiriki
3.00 - 4:00	6.3 Mpango wa mfano Kijiji cha Makundusi (Serengeti): Mawasilisho, Maswali na majibu	Kabange
4.00 - 4:30	Chai	
4.30 – 5:30	6.4 Mpango wa mfano Kijiji cha Ngereiyani (Monduli): Mawasilisho, Maswali na majibu	Kabange
5:30 – 6:30	6.5 Tathmini ya mafunzo	Washiriki
6:30 – 7:00	6.6 KUFUNGA	Washiriki
7:00 – 8:00	Chakula cha mchana	Washiriki
	KUFUNGA MAFUNZO SIKU YA SITA	

Kiambatanisho Namba 2: Orodha ya washiriki wilaya ya Namtumbo

S/No	JINA	TAASISI	WADHIFA
1	LAMECK MFURUKI	Wilaya	Bwana Nyama
2	PETER A. MABULA	Wilaya	Bwana Nyama
3	HUSSEIN R. SUDDY	Wilaya	Bwana Nyama
4	BETIFRIDA J. MALEKELA	Wilaya	Bwana Nyama
5	AMOS MJUNGU	Wilaya	Bwana Nyama
6	ISSA NDOMONDO	Wilaya	Bwana Nyama
7	FARAJI KILAVO	Wilaya	Bwana Maji
8	SIKOYO M.J.	Wilaya	DWE
9	NALIMI MADATA	Wilaya	DGO
10	HEZRON JOBU	Wilaya	DBO
11	YUSTIN MBIRO	Kata ya Magazini	WEO
12	SAID JAFAR	Kijiji cha Magazini	M/Kiti Kijiji
13	AUSI DANDU	Kijiji cha Likusanguse	M/Kiti Kijiji
14	ABDELEMAN SALUM	Kijiji cha Amani	M/Kiti Kijiji
15	NYUNDO S. NYUNDO	Kijiji cha Magazini	M/Kiti Ardhi
16	ISMAIL BANDA	Kijiji cha Amani	Katibu Hifadhi
17	RAFAEL NOMBO	Kijiji cha Magazini	M/Kiti Hifadhi
18	MAGNUS MWANGACHE	Kijiji cha Likusanguse	M/Kiti Hifadhi
19	RAJAB MUSA	Kijiji cha Magazini	VEO
20	PIUS C. NYONI	Kijiji cha Likusanguse	VEO
21	HEMEDI KAJAO	Kata ya Magazini	Diwani
22	MANYONYI SILAS K.	Wilaya	Afisa Ardhi
23	EDWIN MGANI	Wilaya	Mpima
24	NESTORY E. YAMUNGU	Wilaya	Mipango Miji
25	ENOCK P. NDUNGURU	Wilaya	Afisa Kilimo
26	AMBOKILO PAUL	Wilaya	Afisa Mifugo
27	MAJUMBA I.H.	Kata ya Lusewa	Diwani
28	L. Z. MPOMBO	Kata ya Lusewa	WEO
29	ALLY DH. CHIGO	Kijiji cha Msisimo	M/Kiti S/K
30	ZUBERI MILASI	Kijiji cha Msisimo	VEO
31	MUSSA PILLY	Kijiji cha Ligunga	VEO
32	AMANDOS MBUNDA	Kijiji cha Ligunga	M/Kiti Kijiji
33	SAID RASHID GEHO	Kijiji cha Lusewa	VEO
34	JAMES ELEZIAR NCHIMBI	Kijiji cha Amani	VEO
35	WINFRIDI HILORIMUSI NGONYANI	Kijiji cha Matepwende	VEO
36	JACKSON K. MILONGO	Kijiji cha Ligunga	M/Kiti Hifadhi
37	YAZIDU TEMBO	Kijiji cha Matepwende	Katibu Hifadhi
38	ALLY ANDREA NCHIMBI	Kijiji cha Matepwende	M/Kiti Kijiji
39	AMIMU K. MASAMBUKA	Kijiji cha Milonji	M/Kiti Hifadhi
40	SAMBALI H. MTAWILE	Kijiji cha Milonji	M/Kiti Kijiji
41	DAMAS L. FUKO	Kijiji cha Milonji	VEO
42	ALLY ABDALLA KAUSIA	Kijiji cha Lusewa	M/Kiti Hifadhi
43	MATOLA SANDALI ISSA	Kijiji cha Lusewa	M/Kiti Kijiji
44	IDI OSWALD NGONYANI	Kijiji cha Lusewa	M/Kiti Baraza Ardhi
45	ABDALA KWIZOMBE	Kijiji cha Lusewa	Mzee wa Jadi
46	WAIDU R. FRANCIS	Kijiji cha Msisimu	Katibu Hifadhi
47	JORDAN NGONYANI	Tarafa ya Sasawala	Katibu Tarafa
48	SAMWEL MGELA	Wilaya	Afisa Maliasili
49	GEORGE MRISHO	Wilaya	Afisa M/Jamii
50	NSUBISI KAPULA	Wilaya	Ag. Afisa Mipango

Kiambatanisho Namba 3: Orodha ya washiriki wilaya ya Tunduru

S/No	JINA	TAASISI	WADHIFA
1	DAUDA MOH. BOMA	Kijiji cha Marumba	Katibu Hifadhi
2	ABDALA S. MKAWIA	Kijiji cha Marumba	VEO
3	PHILIMON D. HASSAN	Kijiji cha Misyaje	VEO
4	ADIJA ISSA	Kijiji cha Molandi	Katibu
5	MOHAMMED MJAWALA	Kijiji cha Mbatamila	M/Kiti
6	SALUM TELELA	Kijiji cha Molandi	VEO
7	CHALAMANDA SELEMANI	Kijiji cha Mbatamila	Katibu Hifadhi
8	DICKSON A. KOISHWA	Wilaya	DGO
9	ABAS C. B. MANGWALA	Tarafa ya Nalasi	Katibu Tarafa
10	ANGELA A. YAUNDE	Tarafa ya Nampungu	Katibu Tarafa
11	MSENGA SAID MSENGA	Kata ya Marumba	Diwani
12	MOHAMED S. MKULAMBA	Kijiji cha Misyaje	M/Kiti
13	FADHILI K. KANDURU	Kata ya Marumba	WEO
14	ASBATU M. KASAMBI	Kijiji cha Marumba	M/Kiti B. Ardhi
15	ISMAIL HASSAN MKWANDA	Kijiji cha Molandi	M/Kiti
16	SAID RASHID MSUMBO	Kijiji cha Misyaje	Katibu
17	ZUBERI S. ATHUMANI	Kijiji cha Mbatamila	VEO
18	HASANI SAIDI	Kijiji cha Marumba	M/Kiti
19	CHALALE, N.	Wilaya	Mipango Miji
20	YASINI MUHIDINI	Kijiji cha Nampungu	M/Kiti
21	PHANUEL MAGOGWA	Wilaya	Afisa Ardhi
22	MICHAEL MASANGANO	Wilaya	Ag. DWE
23	MOORING C. MACHEMBA	Kata ya Nampungu	WEO
24	KASSIM DINNY	Wilaya	Afisa Maji
25	ISSA A. NGAJIME	Wilaya	Afisa Mipango
26	H. J. MHELELA	Wilaya	Afisa Misitu
27	BROWN P. KAJENJE	Wilaya	Afisa Nyuki
28	DEOGRATUAS F. MAPUNDA	Wilaya	Afisa Kilimo
29	EUSEBIUS C. NGATUNGA	Wilaya	Afisa Uvuvi
30	JONATHAN A. HAULE	Wilaya	Afisa Kilimo
31	MUSSA NDEKA	Kata ya Nampungu	Diwani

Kiambatanisho Namba 4: Tathmini ya mafunzo kwa maswali mbali mbali



Mada zipi zilizojadiliwa ni muhimu sana katika kazi na majukumu yako?

Na	Mada	Idadi ya waliosema
1.	Ushirikishaji katika mchakato wa kutunga na kutekeleza sheria ndogo za za vi	19
2.	Uainishaji wa rasilimali	3
3.	Mchakato wa kuandaa mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi na changamoto zake (kuandaa, kupitisha na kutekeleza)	51
4.	Dhana ya ushirikishwaji katika kupanga mipango shirikishi	26
5.	Mchakato wa uanzishaji miradi shirikishi ya hifadhi ya jamii (ushoroba)	6
6.	Mchakato wa kupata cheti cha ardhi ya kijiji	11
7.	Sera na sheria katika utayarishaji na utekelezaji wa mipango shirikishi	20
8.	Uwiano na uhusiano katika kutenga maeneo kwa matumizi mbali mbali	17
9.	Uandaaji wa ramani ya kijiji kuonesha maeneo yenye mahitaji mbali mbali	2
10.	Muundo wa kisheria na kitaasisi katika kuandaa mpango shirikishi wa kijiji	1
11.	Mfano halisi wa mpango shirikishi wa matumizi bora ya ardhi (sifa za mpar na ramani nzuri)	2
12.	Kuibua miradi kutoka kwenye mpango	5

Ni kwa kiasi gani wawezeshaji wamemudu kazi yao



Ni kwa kiasi gani washiriki wameshirikiana katika mada mbali mbali




Ni kwa kiasi gani huduma za maandalizi, chakula na ukumbi zimekidhi mahitaji ya mafunzo
Asilimia
80
70
60
50
40
30
20
10
0
78
15
0
0
7
Series1
Kiasi kikubw a
Wastani
Kidogo
Kidogo sana
Haw akutaja
Series1
78
15
0
0
7


Ungependekeza mafunzo haya yaendeshwe katika vijiji vingine?
Asilimia
100
80
60
40
20
0
96
0
1
3
Series1
Ndiyo
Hapana
Ikiwezekana
Hawakutaja
Series1
96
0
1
3

Je ungependekeza mambo gani yaboreshwe katika mafunzo kama haya?

Na	Mapendekezo	Idadi ya ya waliopendekeza
1.	Siku za mafunzo ziongezwe (i)-Ratiba isibanwe sana (ii)-Siku ziwe 10 – 14 na mafunzo yaishe saa 9:30 alasiri (iii)-Mada ya kutenga maeneo (mafunzo kwa vitendo) iongezewe siku (iv)-Muda wa majadiliano uwe mwingi ili washiriki wabadilishane uzoefu	25
2.	Vijiji vilivyoachwa kwenye mradi wa ushoroba viongezwe katika mafunzo ya utayarishaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kudhibiti ujangili	2
3.	Posho ya kujikimu iangaliwe upya (i)-Ilikuwa ndogo haikukidhi matarajio (ii)-Madaraja ya malipo ya posho serikalini yafuatwe (iii)-Viwango havikuwa vizuri hasa kwa washiriki waliotoka vijijini (iv)-Itolewe sawa bila kujali madaraja ya vijijini au wilayani	 2 8 11 12
4.	Wageni wengine waalikwe (kama mgeni rasmi, wanahabari n.k.)	2
5.	Mada ya sheria ndogo iboreshwe zaidi	
6.	Mafunzo yatolewe mara kwa mara (kila mwaka) ili yaende kwa watu wengi zaidi	7
7.	Mada za mafunzo kwa vitendo ziongezwe (i)-Field work iwe zaidi ya vijiji viwili (ii)-Mafunzo kwa vitendo yafanyike katika vijiji halisi (iii)-Mafunzo kwa kuona (video) yatumike. Mf video ya mkutano mkuu wa kijiji kupitisha mpango, mikutano ya kata/wilaya n.k.	4
8.	Makabrasha na vipeperushi muhimu viandaliwe na kugawiwa wakati wa mafunzo	3
9.	Askari wa vijiji (Village Game Scouts) na wapima (Land surveyors) nao washirikishwe katika mafunzo	3
10.	Washiriki wapewe vyeti baada ya mafunzo	2
11.	Mafunzo/elimu ya matumizi bora ya ardhi itolewe moja kwa moja kwa wanakijiji na wala si viongozi wa vijiji pekee	2
12.	Vijiji vinavyopakana na vile vya mradi (ushoroba) vipate muwakilishi angalau mmoja mmoja	1
13.	Wazee maarufu vijijini waongezwe katika mafunzo	1

Kiambatanisho Namba 5: Orodha ya Nyaraka Rejea

Hand out Namba 1

SERA MBALI MBALI NA DHANA YA USHIRIKISHWAJI

1 Maagizo ya Sera ya Maboresho (1998)

a) Serikali za Mitaa (Halmashauri na Vijiji watasaidia na kuwezesha ushiriki wa wa watu katika kuandaa na kuteleza mipango ya maendeleo. Kwa mfano dhana ya O &OD, au Mipango Shirikishi ya Matumizi Bora ya Ardhi,
b) Watasidia kuanzisha na kukuza ushirikiano na ubia kati ya Halmashauri/ya Kijiji na vikundi mbalimbali vya kijamii au watu binasfi katika kuharakisha maendeleo.

2 Maagizo ya Sera ya Ardhi (1995)

a) Kuhakikisha usawa katiak mgawanyo wa kupata ardhi kwa wananchi wote,
b) Kuhakikisha kuwa haki za ardhi zilizopo, hasa kwa wakulima wadogo na wafugaji zinatambuliwa kisheria, zinaeleweka na kulindwa na sheria,
c) Kuhakikisha kuwa ardhi inatumika kikamilifu ili kuchangia katika kuleta maendeleo ya haraka ya kiuchumi na kijamii kwa taifa lote,
d) Kudhibiti land degradation kwa ajili ya maendeleo endelevu

3 Maagizo ya Sera ya Mazingira (1992)

a) Kuhakikisha kuwa rasilimali asili zinatumika kwa njia endelevu na kwa usawa ili kukidhi mahitaji ya msingi ya kizazi cha sasa na kijacho bila kuharibu mazingira wala kuhatarisha afya na usalama wa watu,
b) Kuzuia uharibifu wa ardhi, maji, mimea na hewa, vitu ambavyo ni muhimu kwa uhai wa jamii,
c) Kuhifadhi na kuboresha rasilimali za asili na kutengenezwa, zikijumuisha maeneo muhimu na ya kipekee ya ikolijia ya nchi (Tanzania),
d) Kuboresha mazingira ya uzalishaji katika maeneo ambayo ardhi yake imeharibika yakijumuisha maeneo ya vijijini na mijini ili kuweza watanzania wote kuishi katika mazingira salama kiafya, kiuzalishaji na mwonekano mzuri,
e) Kuongeza ufahamu wa watu kuhusu mahusiano yaliyopo kati ya mazingira na shughuli za kimaendeleo, pia kuhamasisha ushiriki wa mtu mmoja mmoja na jamii nzima katika masuala ya kuhifadhi mazingira.

4 Maagizo ya Sera ya Misitu

a) Development of sustainable regimes for soil conservation and forest protection, taking into account the close links between desertification, deforestation, freshwater availability, climate change and biological diversity,
b) To ensure sustainable supply of forest products and services by maintaining sufficient forest area under effective management,
c) Ensure ecosystem stability through conservation of forest biodiversity, water catchments and soil fertility;

5 Maagizo ya Sera ya Wanyama Pori

a) Wildlife resources shall be protected and utilized in a sustainable manner on the basis of careful assessment of natural heritage in flora and fauna fragile ecosystems, sites under pressure and endangered species, with participation of, and benefits to the local communities. EIA studies will minimize environmentally adverse impacts of development projects in wildlife conservation area (e.g. tourist hotels, rail construction).

6 Maagizo ya Sera ya Maji (2002)

a) Usimamizi wa rasilimali za maji unatekelezwa kwa pamoja kulingana na mahitaji mbalimbali,
b) Kuwepo kwa mikakati madhubuti ya kutatua matatizo ya matumizi ya rasilimali za maji,
c) Kunakuwepo ushirikishaji wa walengwa wote katika mipango na maamuzi ya uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji.

Hand out Namba 2

MCHAKATO WA KUANDAA MPANGO WA MAENDELEO WA KIJIJI

Hatua ya kwanza

Wizara husika inatoa taarifa kwa Halmashauri juu ya kiasi cha fedha kitakachotolewa kama ruzuku kwa Halmashauri kwa mwaka wa fedha husika. Ni jukumu la Waheshimiwa Madiwani, Watendaji wa Halmashauri kuziweka Halmashauri zao katika hali ya kustahili kupata ruzuku hizo.

Hatua ya Pili

Halmashauri inatoa taarifa kwa Kata kuhusu kiasi cha ruzuku watakayopata kama mchango wa kutekeleza mipango ya maendeleo. Nakala za taarifa hupelekwa serikali za Vijijini na Mtaa. Wajibu wa kutoa taarifa hii ni wa Mkurugenzi wa Halmashauri husika. Hatua hii ya pili inaonyesha umuhimu wa mawasiliano katika Halmashauri na ngazi za msingi za Serikali ya Mitaa.

Hatua ya Tatu

Serikali za Vijiji/Mitaa wanaanda mipango yao kwa kutumia vikao mbali mbali na kwa kuzingatia kiasi cha fedha kutoka Halmashauri, pamoja na michango ya wananchi na wadau wengine. Hatua hii inategemea utaalamu uliopo katika Kata na uwezo wake kushirikiana na viongozi na watendaji wengine katika kuwezesha mchakato shirikishi wa uandaaji wa mpango wa maendeleo. Ni vizuri pia kwa viongozi wa vijiji na mitaa wakatambua utaalam uliopo kijijini kwao na kuutumia.

Hatua ya Nne

Kamati ya Maendeleo ya Kata (KMK) inapitia mipango ya awali (draft) ya Vijiji na Mitaa na kuainisha miradi inayohusu Kata nzima kama vile barabara, maji, elimu ya sekondari n.k. Vile vile KMK wanakubaliana namna ya kugawa fedha ya ruzuku iliyoahidiwa na Halmashauri.

Hatua ya Tano

Mkutano Mkuu wa Kijiji husika unaandaliwa kujadili mipango kama ilivyoboreshwa na Kata. Ni mkutano mkuu tu ndio una madaraka ya kupitisha mpango shirikishi wa kijiji na bajeti yake kabla ya mipango hiyo haijawakilishwa kwa Halmashauri husika. Pamoja na kwamba wananchi walishiriki katika hatua ya tatu, ni vizuri washiriki pia katika hatua hii ili wachangie katika maamuzi ya namna ya kuweka vipau-mbele na jinsi ya kuchangia na kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali. Malalamiko mengi ya wananchi juu ya michango yanatokana na ushiriki wao mdogo katika kuamua

kiasi, namna na wakati muafaka wa kutoa michango hiyo. Hatua hii ya tano inatoa fursa ya kupunguza tatizo hilo.

Hatua ya Sita

Halmashauri husika inaandaa mpango wake kwa kuzingatia mipango ya vijiji. Mpango huo wa jumla unapitiwa na wataalamu, madiwani na baadaye kwenye mkutano wa RCC (Kamati ya Uratibu ya Mkoa) Hii ni fursa ya kuunganisha maswala au "**interests"** za Kitaifa, Halmashauri na vijiji na mitaa na vitongoji katika mpango mmoja. Hii ni mojawapo ya fursa muhimu ya kushirikisha Serikali Kuu, na ngazi mbali mbali za Serikali za Mitaa.

Hatua ya Saba

Halmashauri inawasilisha mpango wake Wizarani kwa taarifa na kwa kupatiwa fedha za utekelezaji. Muhimu katika hatua hii ni uwezo wa Halmashauri husika kuweka ripoti ya mpango katika hali nzuri ya kitaalamu na kuwasilisha kwa wakati muafaka.

Hatua ya Nane

Wizara ya Fedha inapitia mipango hiyo na inatoa fedha kwa Halmashauri husika. Ni vizuri pia kwa Halmashauri husika kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa hatua hii.

Hatua ya Tisa

Halmashauri husika inatoa taarifa kwa Kata, Vijiji na Mitaa juu ya kiasi cha fedha kilichopatikana ili utekelezaji wa miradi ile inayotegemea ruzuku kutoka serikali kuu uanze.

Ieleweke kwamba upatikanaji wa taarifa juu ya fedha za ruzuku katika ngazi za msing kutasaidia kuifanya jamii kuwa na aria ya kusimamia matumizi ya fedha hizo kwa ukamilifu.

Hand out Namba 3

MCHAKATO WA KUANDAA MPANGO SHIRIKISHI WA KIJIJI

1 Kutoa tamko/nia ya kupangwa (Ku-declare planning area/Nia)

a) Inafanywa na Halmashauri ya Kijiji (Sec 25, Sheria No. 6 ya 2007)
b) Kutangazwa kwa eneo la mipango miji kunaenda sambamba na utambuzi wa mpaka halisi
b) Nia ifahamike kwa wadau wote kwamba wanapashwa kushiriki ili kutoa michango yao ikiwa ni pamoja na kusitisha kwa muda maendeleo au matumizi ya ardhi ambayo yanaweza kuathiriwa au kuathiri mpango
c) Nia ikishatangazwa, mpango unatakiwa uwe umeshaandaliwa ndani ya kipindi ccha miaka miwili toka kutangazwa kwa planning area
d) Kama kuna rasilimali inayopatikana katika Kijiji zaidi ya kimoja, vijiji hivyo vinaweza kuandaa mpango kwa pamoja au resource management sector plan

2 Kuhamasisha wadau na Kuunda Kamati

a) Halmashauri ya Kijiji kuunda Kamati itakayowezesha uandaaji wa PLUM (inahitaji msaada wa Halmashauri ya Wilaya kuhamasisha wanakijiji ili washiriki katika mchakato wa kuandaa hiyo Kamati; Kama Kamati itahitaji kuongezewa uwezo, basi ufanyike utaratibu wa kuwapatia mafunzo)
b) Kamati inaweza kuundwa kwa kuzingatia Sheria Namba 7 ya 1982 (Sect 107 na 108.2)
c) Uundaji wa Kamati uzingatie jinsia, jiografia na uwazi
d) Majukumu ya Kamati in kama yafuatayo (Angalia wajibu na maukumu)

3 Kutathmini Rasilimali zilizopo (Inventory

a) Kutambua rasilimali muhimu kufanikisha maandalizi ya mpango zilizopo kijijini kwa kuwashirikisha wadau wote na kuandaa ripoti. Ripoti hiyo itakuwa na mambo yafuatayo:
   i) Rasilimali asilia zilizopo (ardhi, uoto, maji, hali ya hewa, makazi)
   ii) Nguvu kazi,
   iii) Miundo mbinu muhimu kwa kuandaa mpango,
   iv) Fedha,
   v) Huduma mbalimbali za jamii (facilities)
   vi) Mipango ya maendeleo iliyopo
   vii) Matumizi mbalimbali ya ardhi yaliyopo

4 Kuangalia ubora wa Ardhi (Land suitability assesment)

a) Kuainisha ubora wa maeneo mbalimbali ya ardhi ya Kijiji kwa matumizi mbalimbali. Tathimini hii ya ubora wa ardhi itaambatana na ripoti ya kiufundi (technical report) itakayozungumzia, pamoja na mambo mengine, yafuatayo:
   i) Kuainisha maeneo ya “mifumo ya ikolojia nyeti/sensitive ecosystems”, hali halisi ya rasilimali (physical characteristics), general condition of the land,
   ii) Ubora wa ardhi kwa matumizi yaliyopo na yatakayopangwa,

   Mahitaji ya jamii,

   Tathmini ya athari zinazoweza kutokana na mpango unaoandaliwa,
   v) Taarifa nyingine muhimu kuzingatia hali halisi
   vi) Taarifa ikamilishwe kwa kuwa na ripoti na ramani

MUHIMU:

Ripoti ya utambuzi wa rasilimali zilizopo (inventory) pamoja na uainishaji wa ubora wa ardhi (land suitability) vitawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji ili zijadiliwe na kuboreshwa

Angalizo

a) Sheria No.6, Kifungu 27.2
b) Unatakiwa uwezo wa kuandaa na kuendesha mkutano wa kujadili na kuboresha taarifa
c) Taarifa za vikao pamoja na mahudhurio zichukuliwe kwa umakini

Kama mkutano utapendekeza marekebisho au nyongeza, basi VLUM ifanye kazi ya kuboresha taarifa hizo kabla ya kuendelea na hatua nyingine (supplementary surveys)

5 Kuandaa Mpango

5.1. Kutambua mahitaji ya ardhi ya sasa na baadae/Community needs and future requirements, (Kif 28(1) a-p)

a) Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi unatakiwa kuwa umeshaandaliwa na kukamilika katika kipindi kisichozidi miaka miwili toka eneo husika kutangazwa na mamlaka inayohusika (kwa maana ya Halmashauri ya Kijiji) kuwa eneo la mipango miji (planning area) (Land Use Planning Act, s 33 (1) (a).
b) Kuelewa mahitaji ya ardhi kwa sasahivi (kiuchumi, kijamii na kimazingira)
c) Kujua idadi ya watu na kasi ya kuongezeka kwake (wahamiaji, ukuaji wa ndani)
d) Kuelewa mahitaji ya ardhi ya baada ya-miaka 10 hadi 20 (kiuchumi, kijamii na kimazingira) ikizingatia mipango ya maendeleo iliyopo kwa mfano kama kijiji kinataka kuwa mji mdogo (townwnship), kuzingatia ufugaji nyuki, WMA, eneo la hifadhi (bufferzone) n.k,

e) Halmashauri ya Kijiji inaweza kuamua juu ya muda wa mpango wenyewe kuendelea kutumika kabla haujapitiwa upya (plan review)
f) Kuzingatia viwango (standards) zilizokubaliwa, kwa mfano shule ya msingi hekta ------- (chukua standards mbali mbali kwa mfano njia za malisho)

5.2. Kupendekeza namna ya kutenga maeneo kwa matumizi mbalimbali

a) Kuzingatia mahitaji ya ardhi kwa shughuli mbalimbali (eneo la kilimo, misitu, hifadhi ya maji, makazi, ushoroba, n.k)
b) Kuzingatia hali halisi (existing situation)
c) Kuzingatia land use compartibility
d) Kuzingatia uhifadhi wa mazingira na maeneo ya hifadhi (sensitive areas, beach areas, swamps/ardhi oevu, vyanzo vya maji n.k)
e) Kuzingatia matokeo ya resource assessment
f) Kuzingatia kutenga maeneo ya uma (makaburi, shule, barabara n.k)
g) Mapendekezo yawe kwenye ramani ya matumizi bora ya ardhi

Mambo ya kuzingatia

a) Sheria ya umilikaji na Sheria ya matumizi
b) Namna ya kuweza kutenga ardhi kwa matumizi ya umma

c) Haki za mtu binafsi katika kupanga
d) Fidia na/au resettlement

6 Mchakato wa kupitisha, kutangaza na kuhifadhi mpango (Plan approval process, gazetting/publication and custodianship)

a) Uandaaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi ulishakamilika, mpango huo *utawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji* kuidhinishwa

b) Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji pamoja na ile ya usimamizi wa rasilimali (*resource sector management plans*) itapitishwa/idhinishwa na *Mkutano Mkuu wa Kijiji ndani ya siku 90 toka kuwasilishwa kwa mujibu wa maelekezo ya Mkutano Mkuu.*

c) Mara Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi utakapo idhinishwa/pitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji (iikwa na mabadiliko ama bila mabadiliko), *Waziri anayehusika na Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi atawezesha kutangazwa kwa Mpango huo katika eneo mwafaka* ili watu wafahamu, waweze kuona na kuukagua Mpango huo.

d) Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ukishapitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji na kutangazwa na Waziri anaehusika, *utahifadhiwa na mamlaka husika (planning authority) ambayo kwa ngazi ya Kijiji ni Halmashauri ya Kijiji* ambapo watu wataweza kuomba kuuona mpango kwa gharama (fee) itakayopendekezwa na Waziri.

e) Baada ya Mpango kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji, utawasilishwa *Wilayani (District Planning Authority) ili uingizwe kwenye Mpango Mkubwa wa Wilaya.* Vilevile, Wilaya (District Planning Authority) inaweza kupendekeza marekebisho/mabadiliko kwenye Mpango wa Kijiji ambayo ni mujibu *yafanyike kabla mpango haujapitishwa na kuanza kutumika*

f) Pamoja na mpango kupitishwa na Waziri, unaweza *vile vile kusitishwa endapo Tume ya Matumuzi Bora ya Ardhi itawasilisha kwa Waziri mapendekezo ya kufanya hivyo*. Hii inawezekana endapo kuna ugumu katika kuutekeleza mpango huo, mabadiliko ya matakwa yaliyopelekea kuandaliwa kwa mpango kama vile kubadilika kwa matumizi toka mpango ulipopitishwa, wadau wakitoa sababu za msingi kukataa kutekelezwa kwa mpango au kwa matakwa ya kuurejea mpango (review and evaluation).

Hand out Namba 4

MAJUKUMU YA WADAU MBALIMBALI

1. Wajibu na majukumu ya mmiliki wa ardhi

a) Kutekeleza bila kushurutishwa matumizi ya ardhi ya eneo analomiliki kama yalivyoainishwa kwenye mpango wa kijiji (S. 47(1))
b) Kujua haki zake kwenye eneo analolimiliki na kuzilinda
c) Kutoa taarifa na takwimu
d) Kushiriki kwenye maamuzi (mkutano wa kuwasilisha na kujadili mpango, mkutano mkuu wa kijiji wa kupitisha mpango)
e) Kuhamasisha wanakijiji wenzake

2. Wajibu na majukumu ya kamati ya VLUM

a) Wanasaidia kuandaa mikutano na kuchukua kumbukumbu
b) Saidia kuunda kamati ya VLUM
c) Kuwasiliana na wadau wengine
d) Kuhamasisha wanakijiji
e) Kuainisha na kupanga vipaumbele vya matumizi ya ardhi
f) Kuhakikisha kuna ushirikishwaji katika maamuzi
g) kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi na sheria ndogondogo
h) Kushiriki katika kujadiliana kuhusu mambo ya matumizi ya ardhi
i) Kusaidia katika kutatua migogoro
j) Kuandaa register ya kijiji ya ardhi
k) Kuboresha usimamizi wa ardhi
l) Monitoring and evaluation

3. Wajibu na majukumu ya wataalam wa ngazi za chini kijijini (village technicians)

a) Hawa ni wanakijiji (committed) ambao wanapata mafunzo wakati wa utekelezaji wa mpango katika kuboresha usimamizi wa matumizi ya ardhi,
b) Huendelea kuwasaidia wanakijiji wenzao katika mambo yote yanayohusiana na usimamizi wa matumizi ya ardhi baada ya timu ya PLUM kumaliza muda wake; mfano namna ya kutunza udongo, usimamizi wa misitu, ardhi ya malisho ya wanyama, mpangilio wa makazi na miundo msingi kama vile njia za waenda kwa miguu.

4. Wajibu na majukumu ya Halmashauri ya Kijiji

a) Mamlaka ya kupanga matumizi ya ardhi ya kijiji (kif. 18(1)),
b) Kuliharifu Baraza la Kata (WDC) kuhusu mambo ya mipango ya matumizi ya ardhi ya kijiji (kif. 18(3)),
c) Kutangaza eneo ndani ya kijiji kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi kupitia magazeti yasiyopungua mawili yanayopatikana ndani ya kijiji,
d) Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya utekelezaji. Mpango unaandaliwa ndani ya miaka 2 tangu notisi ya kutangaza eneo la mpango. Wadau wote wa kijiji ni wajibu wahusishwe,
e) Kuhakikisha kuwa malengo ya sheria ya ardhi ya vijiji ya 1999 yanapatikana,
f) Chombo au mamlaka ya kutekeleza sera na maelekezo ya sheria Na. 6 ya 2007,

g) Kuhakikisha kuwa kuna ufuataji na upatikanaji wa maendeleo endelevu ya kimazingira katika kijiji,
h) Kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Kusimamia Mazingira kubuni vigezo vya kulinda mazingira na matumizi endelevu ya raslimali,
i) Kuhakikisha kuna matumizi yenye tija ya ardhi,
j) Kutunza rasilimaliardhi ya kijiji ikiwa ni pamoja na misitu na wanyama,
k) Kuandaa mipango ya rasilimali za ki-sekta kijijini (maji, wanyama, misitu n.k),
l) Kupitia na kutathmini maombi yote ya ardhi ndani ya kijiji kuangalia kama yanaendana na mipango iliyopitishwa ya matumizi ya ardhi na kutoa ushauri kwa mkutano mkuu wa kijiji,
m) Kuwasilisha mpango uliidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji kwenye Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya kujumuishwa kwenye mpango wa wilaya wa matumizi ya ardhi,
n) Kuandaa inventory of planning resources (kif. 26(1)),
o) Kuandaa tathmini ya ubora wa ardhi ya kijiji (land suitability assessment) (kif. 27(1),
p) Msimamizi mkuu wa wa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji na mipango ya ki-sekta,
q) Kuandaa na kusimamia vikao
r) Kuunda kamati pale inapotakiwa,
s) Kuunda sheria ndogondogo na kusimamia utekelezaji wake,
u) Kutoa hati za kimila za kumiliki ardhi

5. Wajibu na majukumu ya Mkutano Mkuu wa Kijiji

a) Kuidhinisha Mamlaka ya kupanga matumizi ya ardhi ya kijiji (Village land use planning authority),
b) Saidia kuboresha mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji
c) Kuidhinisha mpango wa kijiji wa matumizi ya ardhi na mipango ya rasilimali za ki-sekta (kif. 35(1)). Fanyika ndani ya siku 90 tokea kuwasilishwa,
d) Kwa mpango ambao utakataliwa, kutoa taarifa kwa Halmashauri ya Kata (WDC) na Halmashauri ya Wilaya ndani ya siku 14,
e) Saidia kuandaa mikutano na kumbukumbu zake

6. Wajibu na majukumu ya Mtendaji wa Kijiji (VEO)

a) Mratibu na msimamiaji mkuu wa shughuli na maagizo yote ya Mkutano Mkuu wa Kijiji na Halmashauri ya Kijiji

7. Wajibu na majukumu ya Halmashauri ya Kata (WDC)

a) Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji ndani ya kata husika

8. Wajibu na majukumu ya Halmashauri ya Wilaya

a) Mamlaka ya kupanga matumizi ya ardhi ya wilaya (kif. 18(1)),
b) Kwa kushirikisha wadau wote, kuandaa mipango ya jumla ya matumizi ya ardhi ya wilaya. Mpango unaandaliwa ndani ya miaka 3 tangu notisi ya kutangaza eneo la mpango,
c) Chombo au mamlaka ya kutekeleza sera na maelekezo ya sheria Na. 6 ya 2007. (kif. 23)
d) Kuratibu sekta mbalimbali,
e) Kuratibu mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji,

f) Kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Kusimamia Mazingira kubuni vigezo vya kulinda mazingira na matumizi endelevu ya raslimali,
g) Kuandaa *inventory of planning resources (kif. 26(1)),*
h) Kuandaa tathmini ya ubora wa ardhi ya wilaya (*land suitability assessment),* kif.27(1),
i) Msimamizi mkuu wa wa mpango wa matumizi ya ardhi ya wilaya,
j) Kuwasilisha mpango uliidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji kwenye Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya kujumuishwa kwenye mpango wa wilaya wa matumizi ya ardhi.

10. Wajibu na majukumu ya Sekretariati ya Mkoa

a) Kuratibu mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya,
b) Kuandaa mipango ya ki-sekta ya matumizi ya rasilimalikwenye mkoa,
c) Kuunda chombo (*machinery)* cha kuratibu sekta mbalimbali,
d) Kuridhia mipango mipango ya jumla ya matumizi ya ardhi ya wilaya,
e) *Ensure coordination of physical development and systematic land use in each region.*

11. Wajibu na majukumu ya Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi

a) Mamlaka ya kupanga matumizi ya ardhi (kif. 18(1))
b) Mamlaka ya kitaifa ya kupanga matumizi ya ardhi (kif. 19(1))
c) Baada ya idhini ya Waziri, kutangaza eneo kama eneo kwa ajili ya kuandaa mpango wa kanda (zonal) wa matumizi ya ardhi au kuridhia (adopt) mpango uliopo,
d) Kuandaa mpango wa jumla wa kitaifa wa matumizi ya ardhi (kif. 19(2))(a),
e) Kuandaa mipango ya kiundani (detailed) matumizi ya ardhi ya kanda (zonal) (kif. 19(2))(b),
f) Chombo au mamlaka ya kutekeleza sera na maelekezo ya sheria Na. 6 ya 2007,
g) Kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Kusimamia Mazingira kubuni vigezo vya kulinda mazingira na matumizi endelevu ya raslimali,
h) *Ensure coordinated and orderly physical development at the national level,*
i) Kuandaa *inventory of planning resources (kif. 26(1))*

12. Wajibu na majukumu ya Waziri

a) Kuhakikisha kwamba misingi na malengo ya matumizi ya ardhi (kif.3 & 4) yanazingatiwa katika uandaaji wa mipango ya jumla (general) na mipango mchanganuo (detailed) katika mchakato mzima wa uandaaji wa mipango. (kif. 5(1)),
b) Kuidhinisha mipango ya matumizi ya ardhi ya kitaifa, kanda, mikoa na wilaya,
c) Kutoa notisi ya kutangazwa kuhusu kuidhinishwa kwa mipango hadi ule wa kijiji ili wahusika kuona huo mpango katika sehemu na muda utakaokuwa umepangwa,
d) Kukataa mpango wowote uliopitishwa (kif. 38).

Hand out Namba 5

UHAKIKI/TATHMINI YA RASILIMALI KWA MATUMIZI MBALI MBALI

Ardhi na rasilimali nyingine zina matumizi anuwai yanayolenga kufikia malengo mbalimbali ya jamii. Ingawa matumizi haya yako mengi yanaweza kugawanywa katika makundi makuu mawili: *Matumizi bora* na *matumizi holela*. Matumizi bora ni yale:

- Yanayozingatia maslahi ya wadau wote
- Yahakikisha usawa baina ya makundi mbalimbali ya jamii (wanawake, walemavu etc.)
- Yanayolenga kutatua/kupunguza migogoro baina ya wadau mbalimbali
- Yanayolinda mazingira na kuhakikisha uendelevu wa rasilimali (resource sustainability)
- Yenye manufaa makubwa ya kiuchumi (economically rewarding)

1. Lengo la kuamua na kupendekeza matumizi ni:

- kutenga maeneo kuokana na mahitaji ya jamii ya sasa na badae
- kupanga masharti ya matumizi/uendelezaji
- kuoanisha matumizi na milki
- kutoa ramani inayokubalika kitaalamu ambayo baada ya kupitishwa itapelekwa wilayani pamoja na muktasari na maelezo ili kuchangia kuunda mpango wa matumzi bora wa ardhi wa wilaya (sec. 33(b) LUP Act 2007)

Kutokana na wingi wa matumizi ya ardhi na rasilimali, na haja ya kukidhi matumizi yaliyo bora zaidi na kuepuka matumizi holela ni sharti kuzingatia taarifa zilizotokana na uhakiki wa rasilimali husika na kufanya upembuzi kwa kutumia vigezo kadhaa vya kijamii, kiuchumi, kisheria na kiikolojia/kimazingira.

2. VIGEZO VYA KIJAMII (SOCIAL CRITERIA)

- Yabebe ridhaa ya wanakijiji wote (social acceptability)
- Yazingatie vitu ambavyo wanakijiji wanavipa kipaumbele na yasinyime haki za msingi za kijamii k.m. ibada, mila nk.
- Wanakijiji husika wawe na uelewa na utaalamu wa kutosha juu ya matumizi hayo
- Yasinufaishe wanakijiji wachache tu na kuongeza pengo baina ya wanajamii (social imbalances)?
- Yasiwe chanzo cha migogoro baina ya wanakijiji, wadau nk.
- Yasiwe na athari mbaya kwa kina mama: k.m. kuwaongezea mzigo wa kazi, kuwanyima haki ya kumiliki rasilimali, kuwaongezea umaskini wa kipato n.k.

3 VIGEZO VYA KIUCHUMI (ECONOMIC CRITERIA)

- Wanakijiji wawe na uwezo wa kiuchumi (na mitaji) kuwezesha utekelezaji wa matumizi yaliyopendekezwa(economic feasibility)
- Yazingatie unafuu wa gharama katika kuondoa vikwazo, teknolojia inayohitajika, gharama za uzalishaji
- Yawe na manufaa makubwa kiuchumi (economically profitable)
- Yazingatie uhusiano na matumizi mengine (use compatibility)
- Yaboreshe hali za maisha na kuongeza kipato kwa wanakijiji

- Yaweze kuhimili matokeo hasi (risk) k.m. ukame, magonjwa, soko nk.

4 VIGEZO VYA KISHERIA/KISERA/KIASASI (LEGAL/POLICY/INSTITUTIONAL CRITERIA)

- Yazingatie sheria, sera na kanuni zilizopo
- Yazingatie mfumo wa umiliki uliopo (tenure system)
- Huduma muhimu kwa ajili ya uzalishaji ziwepo k.m. huduma za ugani, masoko, mikopo nk

5 VIGEZO VYA KIIKOLOJIA/KIMAZINGIRA (ECOLOGICAL/ENVIRONMENTAL CRITERIA)

Matumizi yanayopendekezwa yasiwe na athari mbaya kiikolojia au kimazingira kama vile kuharibu/kuathiri:

- Vyanzo vya maji
- Udongo
- Hali ya hewa
- Mifumo wa ikolojia (misitu, aridhowevu, na makazi/mapito ya wanyamapori)
- Wanyama na mimea
- Afya za watu nk.

Hand out Namba 6

KUTENGA MAENEO KWA MATUMIZI MBALIMBALI YA RASILIMALI

(RESOURCE USE OPTIONS-sec 28 of LUP Act 2007)

1 Ardhi na rasilimali nyingine hutumika kwa namna mbalimbali ili kukidhi malengo na mahitaji ya watu. Kuyaelewa matumizi haya ni muhimu ili watu waweze:

- Kunufaika zaidi
- Kuhakikisha matumizi yanakuwa endelevu
- Kuhakikisha usawa miongoni mwa wadau
- Kuepuka migogoro

2 Hatua

- Kutokana na uhakiki wa rasilimali na takwimu zingine, chambua kiwango cha maeneo kinachohitajika kwa matumizi mbalimbali (kwa sasa na wakati ujao).
- Oanisha mahitaji haya na kiwango cha teknolojia za uzalishaji na malengo ya maendeleo (uzalishaji). Hii itadhihirisha kama kijiji kina ardhi inayotosha kwa mahitaji yote au hapana.
- Tenga maeneo katika kijiji ambayo yanathamani za kitaifa au yameianishwa katika mipango ya kiwilaya au kitaifa kama ardhi oevu, mapitio ya wanyama, vyanzo vya maji n.k. **INAWEZA KULAZIMISHA KUSITISHWA BAADHI YA MATUMIZI YALIYOPO**
- Kwa maeneo yanayobaki, Angalia matumizi ya sasa matumizi gani hayafai/hayakuabliani kutokana na uhakiki wa rasilimali uliofanyaka, na matumizi gani hayahamishiki kwa mfano makazi, huduma za jamii
- Angalia muelekeo wa kijiji (direction of growth)
- Kwa vijiji vinavyopakana na hiki angalia uhusianao ulipo katika matumizi ya maeneo jirani
- Tenga maeneo katika sehemu baada ya kujiridisha kuhusu yaliyotajwa hapo juu: vigezo ni pamoja na sifa za eneo na utashi wake kwa matumizi hayo (suitability), kukubaliana na matumizi ya sasa (existing uses), kukubaliana na matumizi jirani (compatibility and relations between functions), kukubaliana na ukaribu-ufikwaji wa huduma muhimu kama barabara, makazi (accessibility and easements), milki za eneo (tenure), ukubwa wa eneo, teknolojia inayofaa nk.
- Angalia eneo kama linabaki tenga kwa matumizi ambayo hayaharibu (conservation is also the use).
- Iwapo eneo ni dogo jaribu kubadilisha kiwango cha mahitaji kwa kubadilisha kiwango cha uzalishaji. Hizi huwa ni "a*ssumptions on technology of production*". Angalia pia uwezekano wakupata maeneo sehemu nyingine. Pia kubadilisha shughuli za uzalishaji (alternatives non-natural-resource dependant income generation activities e.g. off farm).
- Angalia matumizi ambayo yanaweza kutumia eneo moja kwa misimu tofauti bila kuleta

mgongano.

- Toa njia za ufikwaji na mahitaji mengine yayohitahika ili eneo litumike kama lilivyopangwa (easements, accessibility, compulsory infrastructure).
- Tengeneza masharti ya uendelezaji: Mara nyingi hutokana na Sheria zilizopo, *assumptions in production technology and uses*, mila na destuli za wanakijiji, muda wa mpango, maeneo jirani na matumizi yake n.k
- Unaweza ukawa na michoro mbadala (alternative-s) na badae chagua moja kulingana na vigezo kama: gharama, kukubalian na hali ya sasa:
- Kupanga miradi inayotokana na utengaji wa meneo ili ijumuishwe katika miradi mikuu ya kijiji (resulting projects to supplement land use plan)

3 USHIRIKI

- Wanakijiji Kuchangia malengo katika matumizi
- Wanakijiji Kutoa mapendekeozo ya meneo au kutathmini mapendekezo
- Wamiliki kukubali mabadiliko ya matumizi ya meneo
- Wamiliki kutoa ardhi kwa matumizi ya jamii
- Wanakijiji Kuchangia katika masharti ya undelezaji
- Wanakijiji Kuweka viwngo vya uendelezaji
- Serikali ya kijiji na wataalamu kuhusianisha mpango na vijiji jirani na mapango wa wilaya wa matumizi bora ya ardhi
- Wanakijiji Kupitisha/kutataa na kubadilisha mpango kataika mkutano wa kijiji

Hand out Namba 7

JAMII NA UHIFADHI (COMMUNITY CONSERVATION)

TARATIBU ZA KUTEUA MAENEO YA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI

Kabla eneo halijateuliwa kuwa Eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori, ni lazima taratibu zifuatazo zifuatwe:

1) Halmashauri ya Kijiji itatoa mapendekezo kwa Mkutano Mkuu wa Kijiji kuhusu sehemu ya ardhi ya kijiji husika inayostahili kuwa Eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori,

2) Chama Wakilishi cha Jumuiya kilichoidhinishwa (AA) kitawasilisha maombi kwa niaba ya vijiji kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori yakiambatana na nyaraka zifuatazo:
   a) Nakala iliyothibitishwa ya kumbukumbu ya Mkutano Mkuu wa Kijiji kuidhinisha kuteuliwa kwa eneo husika; na kumbukumbu hiyo lazima iwe imeshuhudiwa na Afisa aliyeruhusiwa kisheria kupokea viapo na shuhuda,
   b) Taarifa kamili kuhusu yale yaliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni,
   c) Nakala ya cheti cha usajili wa Chama cha Jumuiya na nakala hiyo lazima iwe imeshuhudiwa na Afisa aliyeruhusiwa na sheria kupokea viapo na shuhuda,
   d) Mpango wa Kijiji wa Matumizi ya Ardhi ulioidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji husika,
   e) Rasimu za Mpango wa Jumla wa Usimamizi au Mpango wa Kanda wa Usimamiaji wa Rasilimali

3) Mkurugenzi atakusanya taarifa juu ya eneo linalotarajiwa kuwa Eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori zitakazojumuisha yafuatayo:
   a) Jina la Eneo
   b) Fedha kwa ajili ya kuendeshea eneo
   c) Vitega uchumu (kama vipo)
   d) Shughuli za Kiuchumu (kama zipo)
   e) Shughuli za Maendeleo (kama zipo)
   f) Watendaji katika mradi au programu

4) Mkurugenzi atawasilisha ombi pamoja na mapendekezo yake kwa waziri wa maliasili na utalii

5) Waziri wa maliasili na utalii atatangaza eneo la jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori na kusababisha kuchapishawa kwa chama wakilishi na eneo lililoteuliwa katika gazeti la serekali